SportPesa
TZS. 642,668,240
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Mchakato** ukarabati wa jengo lililoungua Kariakoo waanza UKURASA 2


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Novemba 7, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya

ISSN 0856 • No. 0580757

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




**Harmonize:** Bando lenu, ila potezeeni UKURASA 20



## RIPOTI MAALUM

# Binti mtumiaji shisha asimulia ilivyomponza

• **Fundo** moja ni sawa na sigara 200, aanika hatua tatu akianza na bangi... *Endelea ukurasa 4*

## YALIYOMO


UKURASA WA 3
**MGUU WA MWENYE UALBINO WAPATIKANA**
JESHI la Polisi mkoani Tanga, limeupata mguu wa Heri Kijangwa (45), uliokatwa...

UKURASA WA 3
**HESLB YAFUNGUA DIRISHA LA RUFANI**
BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) jana ilifungua...

UKURASA WA 5
**HOSPITALI 'YALIA' UHABA WATUMISHI**
HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga inakabiliwa na upungufu...


## Auawa kikatili, macho yatobolewa

UKURASA 3




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akihutubia katika maadhimisho ya mwaka mmoja wa uongozi wake, Mkoa wa Mjini Magharibi jana. Kulia ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla na Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman (katikati). **PICHA: IKULU**

# Dk. Mwinyi asema mwaka wake Ikulu ulikuwa mgumu

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA SC YAMTAKA CHAMA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## Mchakato ukarabati Kariakoo waanza

**Na Mary Geofrey**

SIKU chache baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuahidi kutoa Sh. bilioni 32.2 kwa ajili ya ukarabati wa soko la zamani na ujenzi wa Soko la Kariakoo, utekelezaji wake umeanza.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ummy Mwalimu na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Masauni, jana walitembelea soko hilo na kuahidi kuwa mchakato wa kuomba fedha Hazina utakamilika Novemba 15, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari katika soko hilo lililoungua Julai, mwaka huu, Ummy alitoa siku hizo kwa Katibu Tawala wa mkoa huo kukamilisha mchakato wa kupata fedha hizo.

"Tunafahamu hili ni eneo la Jiji la Ilala lakini ninaomba usimamizi wa ujenzi wa soko hili tuhamishie Ofisi ya Mkoa kwa ajili ya utekelezaji na baada ya kukamilika tutaelekezana katika vikao vyetu vya ndani liwe chini ya usimamizi wa nani," alisema Ummy.

Alisema fedha hizo zitatumika katika kukarabati jengo la zamani lililoungua na kujenga jengo jipya la ghorofa sita na mbili kwenda chini katika eneo la soko dogo.

"Soko jipya litakuwa na wafanyabiashara zaidi ya 2,000, hivyo wafanyabiashara wasiwe na wasiwasi, wote watapewa maeneo ya biashara baada ya ukarabati na ujenzi kukamilika," alisisitiza Ummy.

Alisema vikwazo havikosekani lakini miji lazima ipangwe sambamba na kuwapeleka wafanyabiashara katika maeneo yaliyoandaliwa ili kufanya biashara kwenye mazingira bora.

"Lazima miji ipangwe na tunamshukuru Rais Samia amesisitiza lazima miji ipangwe na iwe salama, changamoto hazikosekani lakini tuzitatue, Ninaupongeza Mkoa wa Dar es Salaam kwa jitihada kubwa za kuwapanga machinga," alisifu Ummy.

Naye Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Masauni alisema kuwa kati ya fedha hizo, Sh. bilioni sita zitatumika kukarabati soko la zamani lililoungua na Sh. bilioni 26 zitatumika kujenga soko jipya.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, aliishukuru serikali kwa kuidhinisha fedha hizo na kuahidi kuwa watasimamia kikamilifu kazi hiyo ili ikamilike kwa wakati na kuwaondolea usumbufu machinga.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Machinga, Steven Lusinde, aliiomba serikali kuwaondoa wafanyabiashara wakubwa waliokuwa wanamiliki vibanda nje ya soko hilo ili kutoa fursa kwa machinga ambao ndio walengwa.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu (kulia), akijadiliana jambo na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, walipofanya ziara ya kutembelea Soko Kuu la Kariakoo jana, tayari kuanza kwa mchakato wa ujenzi na ukarabati wa soko hilo, utakaogharimu Sh. bilioni 32.2. **PICHA: MARY GEOFREY**

# Dk. Mwinyi asema mwaka wake Ikulu ulikuwa mgumu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema mwaka wake wa pili wa uongozi utakuwa na mafanikio mengi zaidi kuliko mwaka mmoja wa uongozi wake uliopita ambao ulikuwa mgumu kutokana na janga la corona lililosababisha hali ngumu kiuchumi.

Dk. Mwinyi alibainisha hayo jana alipohutubia wananchi katika sherehe za maadhimisho ya mwaka mmoja wa uongozi wake zilizofanyika katika Hoteli ya Golden Tulip, pembezoni mwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, Zanzibar.

Alisema kuwa mwaka 2020 kasi ya ukuaji uchumi iliporomoka hadi asilimia 1.3 kulinganiswha na asilimia 7.7 ya mwaka 2019 kabla ya ugonjwa wa corona ambapo idadi ya watalii pia ilipungua kwa asilimia 51.6 kufikia watalii 260,0000 mwaka 2020 kutoka watalii 538,0000 mwaka 2019.

Rais Mwinyi alisema asilimia 95 ya hoteli za Zanzibar zenye hadhi ya nyota moja hadi tano zilifungwa mwaka 2020 kutokana na corona na kusababisha kupunguzwa kwa wafanyakazi wakati maendeleo ya utalii yamefungamana na maendeleo ya ukuaji wa sekta nyingine.

Alisema kuwa kutokana na kuanguka huko kwa utalii, sekta zingine zilikumbwa na mdodoro wa uchumi na kusababisha kupungua kwa mzunguko wa fedha katika uchumi wa nchi.

Alisema serikali yake inatarajia kukopa fedha Sh. bilioni 230 kwa ajili ya kuimarisha sekta na maeneo mengine ambayo hayamo katika fedha za mkopo wa IMF, ambapo shirika hilo limeipatia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Sh. bilioni 230 kwa ajili ya kupambana na UVIKO-19.

Alisema fedha hizo zitatumika katika maeneo maalum ikiwamo ujenzi wa miundombinu na uwezeshaji wa wajasiriamali.

Dk. Mwinyi alisema kuendelea kufufuka kwa uchumi wa dunia na kuimarika kwa uchumi wa Zanzibar hasa katika sekta ya utalii kunampa imani kubwa ya kuhimili mkopo huo ili kufanya mambo makubwa kwa wananchi.

Alisema fedha hizo atakazokopa zitatumika kuongeza mzunguko wa fedha kwa wafanyabiashara na wananchi na katika mwaka wa pili wa uongozi wake, atahakikisha analipa madeni makubwa ambayo serikali inadaiwa na wazabuni, malipo ya fidia ya mali za wananchi, malipo ya wastaafu na wafanyakazi wa serikali.

Alisema serikali inapochelewesha kulipa madeni kwa wazabuni na wafanyabiashara inaathiri mitaji yao na hivyo kuathiri ukuaji wa biashara na mzunguko wa fedha.

"Tukiwa na mipango imara ya kulipa madeni haya, shughuhli nyingi za kiuchumi na kijamii zitaimarika kwa sababu kutakuwa na kiwango kikubwa zaidi cha fedha katika mzunguko," alisema.

Aliongeza kuwa moja ya athari kubwa zilizosababisha mzunguko wa fedha kupungua katika uchumi ni sakata la kampuni ya Master life ambayo ilikusanya Sh. bilioni 38.7 kutoka kwa wananchi wapatao 10,317, wengi wao wakiwa ni wananchi maskini na kupelekea wananchi kupata matatizo ya kiuchumi.

Alisema serikali imefanya uamuzi wa kuwalipa wananchi walioweka fedha zao katika kampuni hiyo baada ya kufanya uhakiki, lengo likiwa kuwasaidia kimaisha kwa kuwa wameathiriwa na tatizo hilo la kitapeli.

"Serikali itaendelea kukamata mali za kampuni ili kufidia fedha zitakazotolewa na serikali na hadi sasa kiwango cha Sh. bilioni 6.7 kutoka katika akaunti za viongozi wa kampuni hiyo kimepatikana," alisema.

Alisema ameamua kubeba suala hilo ili kuwaondoshea usumbufu wananchi wanaoupata kutokana na kuweka fedha zao katika taasisi hiyo na fedha hizo watakaporudishiwa zitaingia katika mzunguko na kukuza uchumi wa nchi.

Alisema ili kufanikiwa katika azma hiyo ya mwaka mmoja unaofuata, lazima kudumisha amani iliyopo kwa kuwa ndani ya jamii yameshaanza maneno yanayoashiria uvunjifu wa amani.

Aliwasihi viongozi kuwa nchi ina amani, mshikamano na umoja, hivyo asitokee mtu akaichezea.

Alisema ili kufanikiwa lazima kuwe na uwajibikaji ambapo kila mmoja anapaswa kuwajibika.

Alisema eneo lingine la kulifanyia kazi ili kufanikiwa ni uadilifu, akionya kuwa ukikosekana, fedha za umma zitaingia mifukoni mwa watu wachache.

"Ninatoa tahadhari fedha hizi hata senti moja isipotee, nikisikia kuna mtu kala rushwa katika tenda, basi jihesabu kabisa kwanza kazi utakuwa huna lakini pia tutakushtaki. Ndugu zangu miradi mingi haikufanyika vizuri kwa sababu ya rushwa," alionya.

Dk. Mwinyi alisema ameshapata taarifa za kuwapo baadhi ya watu waliojipanga kutafuna fedha hizo, akionya kuwa hakuna hata senti moja itakayoliwa.

Alimshukuru Rais Samia kwa kumpa ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yake na jitihada zake za kuwezesha kupata mkopo wa kupambana na athari za UVIKO-19 ambazo zitawezesha miradi mbalimbali.

"Ninataka leo niseme hadharani, Rais Samia amekuwa karibu mno na mimi kila changamoto ninazompelekea zote amezifanyia kazi na anafuatilia mambo yetu na anatukia mema na nataka nimwahidi nitaendelea kufanya kazi naye bega kwa bega," alisema.

Akizungumzia baadhi ya mafanikio katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wake, alisema amani, umoja na mshikamano imetawala Zanzibar na kuwezesha kukuza uchumi, huduma za jamii na kuhamasisha uwekezaji.

Alisema ukusanyaji wa mapato kwa Novemba 2020 hadi Septemba 2021 umefanikisha kupatikana jumla ya Sh. bilioni 710.8, sawa na asilimia 69 ya makadirio ya kukusanywa Sh. trilioni moja, ambapo makusanyo hayo ni ongezeko la asilimia 24 kulinganishwa na makusanyo Sh. bilioni 572 kwa kipindi cha Novemba 2019 hadi Septemba 2020. Akitoa salamu zake kwa njia ya simu, Rais Samia Suluhu Hassan, alisema ili kujenga Zanzibar moja, ni lazima wananchi kushirikiana na kuwa wamoja ili kumpa nguvu Rais Dk. Mwinyi kuiletea maendeleo Zanzibar.

Sherehe hizo zilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, vyama vya siasa na mabalozi kutoka nje ya nchi wanayoiwakilisha Tanzania. Viongozi wastaafu; Jakaya Mrisho Kikwete, Dk. Ali Muhamed Shein, Dk. Amani Abeid Karume, Dk. Muhamed Gharib Bilali, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Maoud na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah, ni miongoni mwa walioshiriki.

HABARI KITAIFA

# Kijana auawa, atobolewa macho

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KIJANA anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka 25-30 ambaye hajafahamika kwa jina wala makazi yake, amekutwa ameuawa na kutobolewa macho katika ghuba la kuhifadhi taka la Ngokolo Mitumbani, Manispaa ya Shinyanga.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mwinamila katika eneo hilo la tukio, Amir Athumani, alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana.

Alisema kuwa baada ya kufika eneo la tukio majira ya saa moja asubuhi, waliukuta mwili wa kijana huyo, ukioneka ametobolewa macho na watu ambao bado hawajafahamika.

"Tukio hili ni la pili la watu kuuawa kwenye ghuba hili. Tukio la kwanza ni mtoto mdogo aliyeuawa na kuweka ndani ya boksi. Tunaomba wananchi kama wana migogoro, watafute ufumbuzi na kuacha kujichukulia sheria mkononi," alisema.

Kiongozi huyo alisema kuwa watu mbalimbali walifika kwa lengo la kumtambua kijana huyo, lakini hakuna aliyemtambua na jitihada za utambuzi zilikuwa zinaendelea.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, George Kyando, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kubainisha kuwa bado wanafanya upelelezi ili kuwabaini waliotekeleza mauaji hayo na kiini chake.

Alisema kuwa kwenye eneo la tukio, Jeshi la Polisi lilikuta vyuma pembeni ya mwili wa kijana huyo na kuna hisia ndivyo vilitumika kutekeleza unyama huo.

Kamanda Kyando alisema mwili wa marehemu umehifadhiwa kwenye chumba cha kuhifadhi maiti cha Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga.



Askari polisi wakiupakia kwenye gari mwili wa kijana aliyekutwa ameuawa na kutobolewa macho na watu wasiojulikana na kutupwa katika ghuba la kuhifadhia taka, eneo la Ngokolo Mitumbani, Manispaa ya Shinyanga usiku wa kuamikia jana. Mwili huo, ulipelekwa katika Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga kwa hifadhi na uchunguzi zaidi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mguu wa mwenye ualbino wapatikana

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi mkoani Tanga, limeupata mguu wa Heri Kijangwa (45), uliokatwa na baadaye kufichwa kwa kufukiwa ardhini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Tanga, Safia Jongo, alisema mwili huo ulifukuliwa Wilaya ya Lushoto Oktoba 26, mwaka huu.

"Tulipata taarifa kuwa kaburi la Heri limefukuliwa baada na ndugu kwenda kaburini na kukuta limetitia.

Kamanda Jongo alisema Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya ya Lushoto walifika eneo hilo na kulifukua na kukuta mwili wa marehemu upo isipokuwa mguu wa kulia umekatwa.

Alisema Jeshi la Polisi lilianza upelelezi na Novemba Mosi, jioni walikamata watu watatu ambao walikiri kushiriki kwenye tukio hilo la kufukua kaburi na kukata kiungo hicho kwa kushawishiwa na mtu ambaye hadi sasa anatafutwa.

"Walitupeleka eneo ambalo wamefukia kiungo hiki na kulifanikiwa kukipata. Wito kwa wananchi waondoe taharuki kwa ndugu zetu wenye ualbino. Mkoa wa Tanga hauna kabisa matukio ya aina hii kwa watu wenye ulemavu wa ngozi, hata kwenye familia hii ambayo mwenye ualbino amefukuliwa, wapo wengine wawili na wanaishi kwa amani.

"Katika mahojiano na watuhumiwa wamekiri kwamba ni mambo ya vijiweni ya kwamba ukiwa na kiungo cha mwenye ualbino kwenye nyumba, utajiri utakufuata," alisema.

Kamanda huyo aliwataka wananchi kutumia tukio hilo kama funzo na waache kudanganyana na kushawishiana.

"Wenye vyombo wanaotumia wenye ualbino kusema kwamba Tanga sasa wenye ualbino hawako shwari, hapana! Wapo salama na Tanga vitendo hivi havipo, hata tukio hili lilotokea ni mtihani tu siyo mganga.

"Watuhumiwa hawa wanakiri ndiyo maana wakaonyesha mahali walikofukia, hii ina maanisha kwamba walikuwa hawana pa kukipeleka." alisema.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Mwanzilishi na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika lisilo la kiserikali la Under the Same Sun nchini Canada, Peter Ash, alitoa taarifa kwa umma kulaani tukio hilo na kueleza kuwa Heri alifariki dunia Julai 4, mwaka huu kutokana na saratani ya ngozi na mwili wake ulizikwa siku iliyofuata katika Kijiji cha Tandwa wilayani Lushoto.

Ash alisema shirika hilo lilimsomesha kijana huyo na kabla ya umauti, alikuwa anachukua Shahada ya Uzamili ya Afya ya Jamii katika Chuo Kikuu cha Muhimbili, akiwa amemaliza Shahada ya Kwanza ya Sayansi ya Kimataifa na Teknolojia mwaka 2015.

Pia aliiomba Serikali ya Tanzania kuongeza jitihada za kudhibiti saratani ya ngozi kwa kundi hilo.

## HESLB yafungua dirisha la rufani

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) jana ilifungua dirisha la rufani ili kuwawezesha waombaji ambao hawajapangiwa mikopo au wanahitaji kuongezwa viwango vya mikopo kwa mwaka wa masomo 2021/22 kuwasilisha maombi ya rufani zao.

"Dirisha hilo litakuwa wazi kwa siku tano kuanzia leo (jana) Novemba 6, hadi 10, 2021 na ni fursa kwa wanafunzi wote, wa mwaka wa kwanza na wanaoendelea kuwasilisha maombi yao ya kuongezewa viwango vya mkopo au kupangiwa kwa wale ambao hawajapangiwa hadi sasa," alisema Dk. Veronica Nyahende, Mkurugenzi wa Uchambuzi na Upangaji Mikopo wa HESLB.

Kuhusu utaratibu wa kuwasilisha maombi ya rufani, Dk. Nyahende alisema maombi yote ya rufani yanapaswa kuwasilishwa kwa njia ya mtandao kama yalivyowasilishwa maombi ya msingi.

"Kupitia dirisha hili, tunawasihi waombaji mikopo kusoma maelekezo kwa makini na kuyazingatia, ikiwamo kuweka nyaraka zinazothibitisha uhitaji wao ambazo awali hawakuwa wameziweka," alisema.

Dk. Nyahende alifafanua kuhusu wanafunzi wanaoendelea na masomo na ambao walikuwa wameomba mkopo kwa mwaka 2021/22 kuwa maombi yao yamechambuliwa na wale wenye sifa tayari wameshapangiwa mkopo.

"Hawa tunawaita 'first time continuing applicants' na tumeshawapangia na kuweka taarifa zao katika SIPA na kwa kuwa ni wazoefu, wakiingia wataona, maofisa mikopo wa vyuo pia wana taarifa zao," alisema Dk. Nyahende.

Kuhusu malipo ya fedha kwa wanafunzi waliopangiwa mikopo, Dk. Nyahende alisema HESLB imeshatuma vyuoni fedha za wanafunzi wote wa mwaka wa kwanza ambao wamepangiwa mikopo na kuwakumbusha wanafunzi hao kufika katika ofisi za mikopo vyuoni ili kukamilisha taratibu za kupokea fedha hizo.

RIPOTI MAALUM

## FUNDO MOJA, SIGARA 200...

# Binti mvutaji wa shisha asimulia alivyoharibikiwa

Na Romana Mallya

- Maisha ya barazani jioni yamponza
- Alianza kwa macho, siku alipojaribu...



Mwanamke akivuta shisha

NI hali ya kusikitisha ingawa inabaki palepale kwamba ndio hali halisi. Kisa na mkasa cha mwanamama kijana anayejitambulisha kuwa ni mtumiaji dawa za kulevya, akiweka msimamo kuwa hawezi kuacha wala hana mpango huo.

Akiwa mwenyeji wa Nipashe kwenye mazungumzo maalum, Rehema (siyo jina lake halisi), mkazi wa Sinza Kumekucha mkoani Dar es Salaam, kwa sasa yupo katika awamu ya tatu ya matumizi ya dawa za kulevya aina ya sheesha (shisha), anakiri anachokitumia sasa, ndio hasa kinampatia kile atakacho kwa asilimia zote.

Rehema ambaye ni mchangamfu na anayejiamini, anataja hatua ya kwanza kwamba alianza na bangi, tena kwa kuiga, kisha akahamia kwenye sigara kabla ya kujisogeza katika uvutaji wa shisha, anayoipa cheo haina mpinzani, akijinasibu inampa raha aitakayo na hatoiacha ng'o!

Ameingiaje kwenye urahibu huo? Rehema ambaye kwa sasa hana kazi maalum baada ya kuachishwa kwenye taasisi binafsi (anaitaja), anasimulia mwanzo wa safari yake mwaka 2019, akiwa mkazi wa Kariakoo katikati ya Mtaa wa Livingstone na Congo, alijikuta anaingia kwenye mkumbo wa kuvuta bangi kutokana na mazoea ya majirani aliokuwa akishinda nao barazani jioni baada ya kazi.

Kwa mujibu wa dada huyo mwenye umri miaka 23 sasa, wakati huo anaanza alikuwa 'kijana mbichi' wa miaka 21, akawa mwanachama rasmi wa 'Kariakoo barazani', akipata elimu ya kina ya matumizi ya bangi.

Rehema anasema wakati huo kila alipokuwa akitoka kazini baada ya kupumzika jua lilipotua, ilikuwa ni desturi kwa wakazi wa mitaa hiyo kukaa vibarazani kubadilishana mawazo na hapo ndipo alipoanza kujifunza taratibu bangi.

"Nilikuwa ninawaona vijana wenzangu waliokuwa majirani zangu Kariakoo wanapokaa barazani jioni, wanatengeneza misokoto ya bangi kisha wanaanza kuvuta, nikavutiwa nao nikawa ninawaomba ninavuta.

"Baada ya muda nikazoea nikawa teja, yaani kila nilipojisikia kutamani kuacha nilishindwa maana kuna wakati yaani si umeshapata 'ka-kiu' kunywa pombe, basi nami nikawa ninapata kiu ya kuvuta bangi. Nilijiwekea utaratibu nikiwa ninavuta mara mbili kwa wiki na uvutaji wangu ulikuwa ni kuanzia jioni kabla sijaenda kwenye starehe zangu," anasimulia.

Binti huyo anasema amedumu kuwa mvuta bangi kwa takriban miaka miwili, taratibu akajikuta ndani ya mtiririko wa awamu nyingine ya kuanza kuvuta sigara, ingawa anakiri haikuwa kila mara.

Ndani ya safari hiyo, kuanzia mwaka jana akajitosa kwenye aina tofauti, akivuta shisha, burudani yake anayoisifia inamkosha zaidi kuliko zote zilizotangulia. Anasema kwa mara ya kwanza alipoona watu wanaivuta klabu, alitamani kujaribu kujua ilivyo.

Akirejea alikotoka, Rehema anasimulia alipokuwa katika awamu za bangi na sigara, staili ya matumizi yake haikuishia katika 'kijiwe' barazani pekee, bali aliendeleza penye kumbi za starehe na hasa klabu za usiku alikopenda kwenda siku nyingi.

Huku akifafanua hadi sasa anavutia huko kilevi chake cha sasa - shisha, anakiri kuwa kama ilivyokuwa barazani, huko nako kuna wadau wengine wavutaji ambao wamezama zaidi kwenye shisha, wengi ni vijana wenzake.

"Nimejikuta nami nimezama huko. Kwa sasa nimehamia kwenye shisha, kila nikienda klabu lazima nitafute Sh. 10,000 hadi 25,000 kwa ajili ya kuvuta shisha.

"Shisha ina gharama kidogo. Zipo klabu nyingine zinaiuza mpaka Sh. 60,000 na kuendelea. Nikitoa Sh. 10,000 tunakaa watu watatu kila mmoja akiwa amelipa, tunavuta kwa kutumia mirija maalum. Tunavuta, tunajisikia raha, ni ulevi ambao ukitoka nje kwenye hewa nyingine unajisikia poa," anasimulia.

Rehema ana ufafanuzi kuhusu ulevi huo anaosisitiza umewateka vijana wengi, kwamba wanapenda shisha kwa sababu imetengenezwa kwa kuwekewa ladha tofauti zinazowavutia.

"Ipo yenye ladha ya minti, strobери, ladha ya ndizi na kama zilivyo bia, shisha nayo imewekewa kiwango cha ulevi, zipo zenye kiwango kikubwa cha ulevi na cha kiasi," anafafanua.

**MADHARA YA SHISHA**

Binti huyo anakiri kuwa, hafahamu kemikali na malighafi zilizomo ndani yake na kama zina madhara kiafya.

Hata hivyo, ripoti ya utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Duniani (WHO) mwaka 2019 kuhusu athari za tumbaku na sigara za kielektroniki (ikiwamo shisha), ilibaini sigara za kielektroniki zina kiwango kikubwa cha nicotine, kemikali ambayo ni chanjo cha maradhi ya saratani ya mapafu na magonjwa ya moyo.

Kamishna wa Kinga na Tiba kutoka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Dk. Peter Mfisi, ana angalizo katika hilo, akionya: "Dawa za kulevya zipo za aina mbili; halali na zisizo halali ambazo zinadhibitiwa. Mfano, heroine, cocaine mirungi, bangi na nyingine, tunafanya kazi ya kuzidhibiti, zimeorodheshwa kwenye jedwali. Vitu kama pombe, tumbaku, kuberi vinalevya lakini havidhibitiwi na sheria yetu namba 5 ya mwaka 2015 ya kudhibiti dawa za kulevya."

Anasema Wizara Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilifanya utafiti kuhusu shisha na kubaini ina kiwango kikubwa cha nicotine.

"Mtu akivuta shisha mara moja ni sawa umevuta sigara 200. Wizara ya Afya ililiona hilo, ikaomba mamlaka zinazohusika ikatazwe," anasema na kukiri hadi sasa hakuna sheria inayozuia matumizi ya shisha nchini, hivyo mamlaka yao kushindwa kudhibiti mwenendo wa biashara na matumizi yake.

Kamishna Mfisi katika himitisho lake, anaishauri serikali kuchukua hatua kwa kupeleka muswada wa sheria bungeni kudhibiti biashara na matumizi ya shisha nchini, akibainisha kuwapo vijana wengi wanaovuta shisha kwenye miji mikubwa nchini.

**WIZARA YAKIRI TATIZO**

Meneja Mpango wa Taifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza wa Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Omary Ubuguyu, anasema matumizi ya shisha yana madhara makubwa kiafya.

"Tumbaku unayoichemsha ili uisisimue mwili maana yake ni kwamba mtu anayetumia shisha anamzidi anayetumia tumbaku ya kuvuta kwa maana ya athari za kemikali zinazosababisha sumu ni kichocheo cha magonjwa yasiyoambukiza kama saratani za aina zote.

"Kuharibika mishipa damu na kuongeza hatari ya kuharibu figo na moyo. Matumizi ya shisha ni mlango wa matumizi huria ya dawa za kulevya, wengine wana tabia ya kuchanganya ndani yake cocaine, heroine na bangi. Kubwa kuliko yote ni madhara yake mtu ana uwezekano mkubwa wa kupata matatizo ya saratani, kisukari, figo na moyo," anafafanua.

Dk. Ubuguyu anasema ipo Sheria ya Kuzuia Matumizi Holela ya Tumbaku ya Mwaka 2004, lakini wakati inatungwa shisha haikuwa sehemu ya bidhaa za tumbaku zilizokatazwa kwa mujibu wa sheria hiyo.

"Bahati nzuri, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imepewa jukumu la udhibiti na matumizi ya tumbaku. Hao wana nafasi ya kusaidia.

"Kwenye hili la matumizi ya shisha ni kama umenipa taarifa, nitawakumbusha TMDA kulipitia hilo kisheria kwa sababu wamepewa mamlaka ya dawa na vifaa tiba," anasema.

Nipashe inafika mezani kwa Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa TMDA, Gaudensia Simwanza, ambaye katika ufafanuzi wake anasema tangu Aprili 30, mwaka huu walipokabidhiwa rasmi majukumu ya kudhibiti matumizi holela ya tumbaku, wameanza kwa kutoa elimu kwa umma ili kupunguza idadi ya waathirika wa bidhaa za tumbaku, ikiwamo shisha.

**VIFO KWA MAMILIONI**

Mei 31, mwaka huu, Waziri wa Afya, Dk. Dorothy Gwajima, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kutotumia Tumbaku Duniani, alibainisha kuwa takribani watu milioni sita hufariki dunia kila mwaka kutokana na matumizi ya tumbaku na bidhaa zake kama sigara na shisha na wakati mwingine kuvuta moshi unaotoka kwa mvutaji huku baadhi yao wakiwa ni watoto ambao hupoteza maisha kwa asilimia 28, wanawake asilimia sita na wanaume asilimia moja.

Waziri alirejea ubashiri wa kisayansi kwamba vifo vitokanavyo na matumizi ya tumbaku vitaongezeka na kufika zaidi ya milioni nane kwa mwaka ifikapo 2030, ambao ni mwaka wa ukomo wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Vilevile, takwimu za WHO za mwaka 2003 zinaonyesha kila baada ya sekunde 10, mtu mmoja hufariki dunia kutokana na matatizo yanayosababishwa na matumizi ya bidhaa za tumbaku.

Kwa lugha rahisi ya mazungumzo, hiyo ni sawa na vifo vya watu sita katika kila dakika, sawa na vifo 60 kwa saa na vifo 1,440 kwa siku.

Novemba 3, mwaka huu, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Jakaya Kikwete (JKCI), Prof. Mohamed Janab, akizungumza katika mkutano wa Chama cha Kudhibiti Matumizi ya Tumbaku Tanzania (TTCF), alisema kati ya wagonjwa 100 wa moyo, 25 wanapata maradhi hayo kutokana na matumizi ya tumbaku.

Profesa Jabab pia alibainisha kuwa asilimia 80 ya wanaougua saratani, chanzo chake ni matumizi ya tumbaku.

HABARI KITAIFA

## CCM yahimiza kwa wananchi kudumisha amani

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, amewaomba waumini wa dini ya Kikristo na Waislamu kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika kuendelea kuwaletea wananchi maendeleo nchini huku wakidumisha amani na ushirikiano uliopo nchini.

Vilevile, amewataka waumini hao kuendelea kusimamia na kufuata amri zilizoelekezwa na Mungu kwa kutekeleza mafundisho ya kiongozi wa dini kueneza ujumbe wa amani ulimwenguni.

Alitoa rai hiyo juzi kwenye Maulid ya Mtume Muhamad (SAW) yaliyofanyika katika Madrasat Abbasia jijini Dar es Salaam, akisema ni vyema Watanzania wakaendelea kudumisha amani na upendo huku wakifuata mafundisho ya Mungu.

Alisema ni vyema watu wakaishi na kuufuata mienendo na mafundisho ya Mungu huku wakikwepa vitendo viovu kama dhulma, kusengenyana na kutoishi kwa kuchukiana.

"Kila binadamu amhimize mwenzake katika kutenda haki na kutimiza wajibu ikiwamo kujiweka mbali na matendo maovu ambayo Mungu huchukizwa nayo.

"Mkusanyiko huu mkubwa mnaona unafanyika hapa leo ni kutokana na nchi yetu ina amani, hivyo tujue yapo mataifa kadhaa duniani yanatamani watu wake wakusanyike pamoja kama sisi lakini haiwezekani kwa kuwa hakuna amani katika nchi zao," Shaka alisema.

Alisema kutokana na kuwapo kwa mazingira mazuri ya ustawi wa amani na umoja nchini, Watanzania hawana budi kuilinda na kuiendeleza amani waliyobarikiwa na Mungu.

"Tuzidi kufanya bidii na kukithirisha ibada zetu misikitini na makanisani kumwomba Mungu aijalie neema na fanaka nchi yetu, azidi kutunza na kudumisha amani iliyopo nchini na endapo kuna mwenye shari zake au uchochezi wowote, Mungu mkarimu azivunje nia na dhamira zao batili," alisema.

Alisema ni vyema jamii iendelee kukemea vitendo viovu visivyompendeza Mungu ambavyo kwa aina moja au nyingine vinaweza kuleta machafuko ya amani iliyopo nchini.

Naye Mufti Abubakar Zubeir aliwasihi waumini wote wa Kiislamu nchini kuendelea kuchanja chanjo ya Uviko-19 ili kuendelea kuongeza kinga katika kupambana na ugonjwa huo hatari.

Pamoja na hayo Mufti alisisitiza waumini na Watanzania wote kuendelea kudumisha mshikamano na kushirikiana na serikali katika ujenzi wa taifa.

# Hospitali 'yalia' uhaba watumishi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga inakabiliwa na upungufu wa watumishi 689, sawa na asilimia 65 ya mahitaji, ikiwa na watumishi 241 kwa sasa.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Luzila John, alibainisha hayo juzi alipowasilisha taarifa ya mkoa kwenye uzinduzi wa Bodi Mpya ya Ushauri ya Hospitali hiyo.

Alisema moja ya vikwazo vikubwa ambavyo vinawakabili kwenye hospitali hiyo ni upungufu mkubwa wa watumishi wa afya, hasa kwenye idara ya uuguzi, huduma za kibingwa katika fani za upasuaji na mifupa.

"Katika kukabiliana na changamoto hii, jumla ya madaktari watano tumewapeleka masomoni, wakisomea fani za kibingwa, daktari wa upasuaji wa mifupa yupo KCMC, daktari bingwa wa macho yupo mwaka wa pili sasa shuleni. Pia tuna daktari wa magonjwa ya ndani na daktari wa magonjwa ya dharura."Licha ya kukabiliwa na changamoto hizi za upungufu wa watumishi, katika robo ya mwaka wa kwanza (2021/22) tumetoa huduma ya matibabu kwa wagonjwa 19,832 ndani ya miezi mitatu na kinamama 570 wamejifungua katika hospitali yetu, wakiwamo 244 waliojifungua kwa njia ya upasuaji. Na katika robo hii hakuna kifo cha mama na mtoto kitokanacho na uzazi,"alifafanua.

Kiongozi huyo pia alibainisha hospitali hiyo kupitia fedha za mkopo wa IMF, imetengewa kiasi cha Sh. bilioni 4.5 kwa ajili ya kujenga chumba cha uangalizi maalum (ICU), chumba cha CT-SCAN, EMG na kununua mashine ya CT-SCAN, ili kuondoa kikwazo wagonjwa kupewa rufani kwenda Bugando jijini Mwanza kwa kukosa huduma hizo Shinyanga.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Faustine Mulyutu, alisema Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga pia inatarajia kukopa mashine ya kuchujia figo kutoka katika Bohari Kuu ya Dawa (MSD), ili kuendelea kuboresha huduma za matibabu kwenye hospitali hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, aliwataka watumishi hao wachache katika hospitali hiyo kufanya kazi kwa uzalendo, ufanisi, umoja, kushikamana ili kuendelea kuokoa afya za wananchi wakati serikali ikiendelea kutafuta ufumbuzi wa upungufu huo wa watumishi.

Pia aliitaka bodi hiyo mpya ya ushauri katika hospitali hiyo kufanya kazi yake kwa ufanisi kuishauri menejimenti ya hospitali na kutafuta misaada mbalimbali kuisadia serikali kuboresha huduma za afya katika hospitali hiyo ikiwamo upatikanaji wa vifaa tiba na ujenzi wa majengo mapya.



Mtaalamu wa Macho kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Pwani Tumbi, Maymarina Sway (kushoto), akipima uwezo wa macho kuona karibu kwa Renalda Mosha, ili aweze kupatiwa miwani, wakati wa kambi maalum ya upimaji macho iliyofanyika katika Kituo cha Afya cha Mlandizi, mkoani humo hivi karibuni. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

# Viwanda 130 vyanufaika KAIZEN

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

SERIKALI imesema viwanda 135 kati ya 80,000 nchini vinanufaika na huduma ya kuimarisha viwanda kwa kuongeza tija katika uzalishaji na ubora wa bidhaa (KAIZEN).

Kufuatia hali hiyo, wamiliki wa viwanda wanapaswa kutambua umuhimu wa matumizi ya falsafa hiyo kwa kuwa inapunguza gharama za uendeshaji.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, aliyasema hayo juzi katika ufunguzi wa kongamano la tatu la wakufunzi wa KAIZEN katika sekta ya viwanda nchini lililofanyika mjini Morogoro.

Alisema matumizi ya falsafa ya KAIZEN ni zaidi ya ubora na tija, na ni zaidi ya kupunguza gharama na upotevu.

"Mabadiliko ya kimsingi yanayoweza kupatikana kutokana na matumizi ya KAIZEN na kuleta matokeo chanya ni pamoja na kubadilika kwa mtazamo wa wamiliki wa viwanda na biashara, mameneja, wasimamizi na wafanyakazi kwa kujijengea hali ya kujiamini na zaidi kujiaminisha kwa wateja na wadau wa mnyororo wa thamani," alisema.

Alieleza kuwa takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa idadi ya viwanda Tanzania kwa sasa ni zaidi 80,000 na kwamba kiasi cha viwanda vilivyonufaika na huduma za KAIZEN kwa kipindi cha mwaka 2013 hadi 2021 ni 135 tu.

"Hii inamaanisha kuwa kasi ya kuenea kwa falsafa ya KAIZEN kwenye sekta ya viwanda nchini bado ni ndogo. Kwa upande mwingine, taarifa ya hali ya uchumi ya mwaka 2020 inaonyesha kuwa uchumi wa taifa letu umekua kwa wastani wa asilimia 4.8 ya Pato la Taifa (GDP).

"Ukuaji huu kwa kiasi kikubwa umechangiwa na sekta ya kilimo (asilimia 26.9), ujenzi (asilimia 14.4) na biashara (asilimia 8.7). Mchango kidogo ulitokana na sekta ya viwanda ambayo ilichangia asilimia 8.4 tu kulinganishwa na asilimia 8.5 mwaka 2019, sawa na upungufu wa asilimia 0.1," alisema.

Vilevile, alisema sekta ya viwanda ilikua kwa kiwango cha asilimia 4.5 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 5.8 mwaka 2019.

"Upungufu huo ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na athari za janga la UVIKO-19. Hivyo, kuna haja kuangalia namna bora ya kuendeleza na kukuza uzalishaji viwandani ili kuongeza fursa za ajira na mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa," alisema.

Aliongeza: "Ni matumaini yangu kuwa matumizi ya falsafa ya KAIZEN yatachangia katika kukabiliana na baadhi ya changamoto zilizopo ili kuondokana na upungufu huo."

Awali, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Viwanda, Lugano Wilson, alisema kati ya viwanda hivyo vilivyonufaika na mafunzo ya KAIZEN, vikubwa ni asilimia 25 na vidogo ni asilimia 75.

'Nina furaha kukwambia kuwa matokeo ya itafiti uliofanywa mwaka 2019 kwa kampuni/taasisi 52 zinazotekeleza falsafa hii ulibaini kuwa asilimia 58 kati yao walikuwa na matokeo chanya katika kudhibiti gharama za uendeshaji," alisema.

Aliishukuru Serikali ya Japani kwa kuendelea kufadhili uenezaji wa falsafa ya KAIZEN Tanzania na kwamba wizara ipo katika hatua za kukamilisha Sera ya Taifa ya Ubora (NQP).

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Wizara ya Ardhi imeonyesha kwa mfano suala la machinga

**SUALA** la wafanyabiashara wadogo, maarufu kama machinga, sehemu mbalimbali nchini limekuwa gumzo kubwa kila kona. Hiyo ni kutokana na mpango na maagizo ya serikali kuwa wanapaswa kuondoka maeneo yasiyoruhusiwa kufanyia biashara baada ya kuwapo sehemu mbalimbali ambazo zinasababisha hata serikali kushindwa kukusanya mapato.

Kinachoendelea sasa kwa wafanyabiashara hao ambao walikuwa wameziba hata njia za waenda kwa miguu katika miji mkubwa, Dar es Salaam ikiwapo, ni kuwahamisha kutoka maeneo hayo huku sehemu zingine nguvu zikitumika.

Sambamba na kuwataka wahame kwa kutii sheria bila shuruti, mamlaka za serikali zimekuwa zikiendesha operesheni ya kubomoa vibanda vya machinga. Kutokana na bomoabomo hiyo, sehemu kadhaa kwenye miji zimekuwa safi tofauti na wiki mbili au tatu zilizopita.

Miongoni mwa mipango ambayo serikali imekuwa ikitangaza katika kuhakikisha kila kitu kinakwenda katika mpangilio ni wafanyabiashara hao wadogo kwenda katika maeneo waliyopangiwa.

Hata hivyo, viongozi wa machinga wamekuwa wakikaririwa na vyombo vya habari kuwa maeneo wanayoamuriwa kwenda ni madogo kulingana na idadi yao. Wengine pia wamekuwa wakionyesha kama wanaikejeli serikali kwamba huko wanakokwenda ni kama likizo na kwamba utafika muda watarejea kwenye maeneo wanayofukuzwa.

Kauli hizo za baadhi ya machinga zinatokana na ukweli kwamba suala la wafanyabiashara hao limekuwa la muda mrefu huku likitawaliwa zaidi na wanasiasa. Wako baadhi ya wanasiasa wakiwamo viongozi wa juu serikalini ambao wamekuwa wakiwakingia kifua kwa madai kuwa ni wapigakura wao, kwa hiyo, hiyo ndiyo jeuri inayowafanya waendelee kutamba kwamba watarudi kwenye maeneo hayo na maisha kuendelea kama zamani.

Licha ya kuwapo kwa ahadi kwamba machinga hao watapelekwa maeneo waliyopangiwa na yanayoendelea kuandaliwa, wiki hii Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilionyesha kwa vitendo namna ya kutafuta suluhu ya tatizo hilo la muda mrefu ili kupunguza, kama si kumaliza, vuta nikuvute hiyo ambayo imedumu kwa miaka mingi.

Wizara kupitia kwa Naibu Waziri, Dk. Angeline Mabula, ilitembelea eneo la Karikaoo kwa lengo la kuangalia namna bora ya kuwawezesha machinga kutumia majengo ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kufanyia biashara.


Hatua hiyo ilitokana na wafanyabiashara hao kuandika barua Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuomba kupatiwa sehemu za kufanyia biashara kwenye majengo ya shirika hilo.

Kutokana na ombi hilo, TAMISEMI iliomba wizara hiyo kuangalia namna ya kuwasaidia machinga kutumia majengo yaliyoko mitaa ya Tandamti na Msimbazi lakini wizara yenye dhamana na NHC iliridhia kwamba majengo yanayoweza kutumika ni matatu yaliyoko Mkunguni na Nyamwezi, hivyo yaboreshwe na kuanza kutumika.

Kwa jumla, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeonyesha mwanga juu ya kutatua tatizo hilo kuwa sehemu na uamuzi huo unapaswa kuungwa mkono na wizara na taasisi zingine za serikali.

Tunasema hivyo kwa sababu suala la machinga ni mtambuka, hivyo kila idara, mamlaka na taasisi za serikali zinapaswa kuwajibika kila moja kwa nafasi yake ili kupatia ufumbuzi suala hilo ambalo kwa sasa ni kama bomu lililotegeshwa na linasubiri muda tu kulipuka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



### Kaulimbiu hii iwe chachu katika kuwabadili madereva bodaboda

Na Sabato Kasika

**MAADHIMISHO** ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani, yanatarajiwa kufanyika kitaifa Jijini Arusha kuanzia Novemba 11 mwaka huu yakiwa na kaulimbiu isemayo " Jali maisha yako na ya wengine barabarani."

Katika maadhimisho hayo, mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan. Pia kutakuwa na utoaji wa elimu na ukaguzi wa vyombo vya moto katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo na viunga vyake.

Hiyo ni kwa mujibu wa Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha, ACP Justine Masejo, katika taarifa yake aliyoitoa kwa vyombo vya habari huku akiwaomba wananchi kujitokeza kwa wingi katika maadhimisho hayo.

Katika taarifa yake, Kamanda huyo anabainisha kuwa, jukumu kubwa la jeshi hilo ni kulinda raia na mali zao, na kwamba kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani Baraza la Taifa la Usalama Barabarani wamekuwa na mpango mkakati wa kutekeleza majukumu yake katika maeneo ya utoaji wa elimu, kufanya operesheni na kusimamia sheria za usalama barabarani.

Ni kweli kwamba, jitihada zimekuwapo za utoaji wa elimu na operesheni mbalimbali na usimamizi wa sheria za usalama barabarani, lakini bado kuna baadhi ya madereva ni wagumu kutii hadi washurutishwe.

Madereva hao ni wa bodaboda, ambao kwao suala la kutii sheria za usalama barabarani ni mtihani mgumu na matokeo yake waendesha vyombo hivyo vya moto watakavyo kana kwamba hakuna sheria zinazowaongoza.

Ni jambo la kawaida kwao, kubeba abiria zaidi ya mmoja, kutovaa kofia ngumu (helmet), kuvuka makutano ya barabara kabla ya kuruhusiwa na taa, hali ambayo inaweza kusababisha ajali.

Kwa mazingira kama hayo, ni wazi elimu zaidi inahitajika kwa kundi hilo, ili kunusuru maisha yao na ya abiria pia, hasa kwa kuwahimiza kuzingaia kaulimbiu ya mwaka huu ya "Jali maisha yako na ya wengine barabarani".

**Kwa mazingira kama hayo, ni wazi elimu zaidi inahitajika kwa kundi hilo, ili kunusuru maisha yao na ya abiria pia, hasa kwa kuwahimiza kuzingaia kaulimbiu ya mwaka huu ya "Jali maisha yako na ya wengine barabarani".**

Mtindo wa kutotii sheria za usalama barabara umekuwa ukielezwa kuwa unasababisha vifo, ulemavu wa kudumu na majeruhi wanaohitaji rasilimali nyingi kwa ajili ya matibabu yao.

Lakini pia matumizi ya vilevi yamekuwa yakitajwa kama sababu kubwa ya matukio ya ajali za bodaboda, hali inayoonyesha wazi kwamba bado kuna haja ya kutoa elimu ya kutosha kwa kundi hilo.

Bodaboda ni moja ya sekta muhimu za usafiri nchini ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia kupunguza changamoto ya foleni nyakati ambazo watu wanahitaji kufika katika maeneo yao ya kazi, shule, hospitali na kwingineko.

Si hapo tu bali inasaidia kupanua wigo wa ajira kwa vijana ambao wako mitaani bila kazi, ingawa baadhi yao wamekuwa si makini katika shughuli hiyo na kusababisha ajali ambazo wakati mwingine ziko ndani ya uwezo wao.

Kwa mfano, mtu haruhusiwi kulewa kisha akaendesha chombo cha moto, lakini kwa baadhi ya madereva wa bodaboda, hawaoni umuhimu huo, badala yake hawajali, wanalewa kama kawaida.

Katika hali hiyo ya kutotii sheria za usalama barabarani, matokeo ni kuendelea kutokea kwa ajali kana kwamba hakuna sheria zinazowakata kuwa makini wanapoendesha vyombo hivyo vya moto.

Mtindo huo wa kutotii sheria za usalama barabarani, uliwahi kumuibua Spika Job Ndugai na kushauri kuanzishwa kwa utaratibu wa kuwachapa viboko madereva wa bodaboda kama inavyofanyika nchini Singapore.

Ni katika kipindi cha maswali na majibu bungeni Dodoma, Aprili mwaka huu anasema, polisi wa nchi hiyo, wanawachapa viboko madereva hao, siyo kuchukua pikipiki na kuziweka vituoni miezi sita kama inavyofanyika nchini.

Wakati nchi inaelekea kwenye maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani, ingependeza iwapo kaulimbiu ya maadhimisho hayo ingezingatiwa na madereva wote wa vyombo vya moto.

## SAFU

### KWA MASLAHI YA TAIFA

# Utapiamlo, udumavu bado ni tatizo



**Na Pascal Mayalla**

TANZANIA bado inakabiliwa na tatizo kubwa la udumavu unaosababishwa na utapiamlo kutokana na kula vyakula vyenye lishe duni. Hadi Juni, mwaka huu, asilimia 31.8 ya watoto chini ya miaka mitano nchini, walikuwa na tatizo la udumavu unaosababishwa na utapiamlo sugu, hatua ambayo imesababisha watoto wachanga kushindwa kukua ipasavyo.

Suluhisho pekee la tatizo hili ni matumizi ya teknolojia ya kisasa ya kibailojia ya kuzalisha mbegu zenye viini ilishe iitwayo, Bayofotifikesheni (Biofortification). Kutokana na suluhisho hilo, umetolewa wito kwa wazalishaji, wasindikaji na wauzaji vyakula kuchukua hatua madhubuti kuboresha mifumo ya uzalishaji ili kuzalisha vyakula vyenye lishe bora.

Ofisa Program kutoka taasisi ya GAIN Tanzania, Mariam Luhambati, kwenye banda la Global Alliance for Improved Nutrition (GAIN), wakati wa maonyesho ya Siku ya Chakula Duniani, yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Pasua, Moshi, mkoani Kilimanjaro, alisema suluhisho ni uzalishaji mkubwa wa mahindi na maharagwe ambayo ndicho chakula kikuu cha Watanzania wengi.

Alisema taifa likifanikiwa kuhakikisha mahindi na maharagwe yote yanayolimwa nchini ni yenye viini lishe, kila Mtanzania na hasa kule vijijini akapata mlo bora na wenye lishe bora, tatizo la udumavu na utapiamlo nchini litakuwa historia.

Luhambati alisema njia ya kufanikisha hilo, ni kwa serikali kusisitiza mbegu zote za mahindi na maharagwe zitakazosambazwa wakulima lazima ziwe ziliiongezwa viini lishe kwa kutumia utaalamu wa kisasa wa utengenezaji wa mbegu (Biofortification). Mbegu hizo zenye viini lishe zinapandwa pamoja na mbegu za kawaida, hivyo zinaota pamoja na kupitia tekinolojia ya kibaiolojia, vile viini lishe kutoka mbegu zenye viini lishe, zinaambukiza zingine zisizo na viini lishe, hivyo mazao yote yanayoota yanakuwa na viini lishe.

Hatua hiyo inatokana na ukweli kwamba 'Biofortification' ni utaalamu wa kuongeza viini lishe vya vitamini na madini katika mazao kwa kutumia utaalamu wa kibayolojia. GAIN kwa ushirikiano na taasisi ya HarvestPlus zinafanya kazi na wadau mbalimbali kupitia Mpango wa Kufanya Biashara ya Mazao Yanayorutubishwa (CBC) ili kuendeleza na kukuza aina za vyakula vikuu vilivyorutubishwa na virutubishi ambavyo kwa kawaida huzalishwa kwa viwango vya juu vya madini ya chuma, zinki au vitamini vyote hivyo vinahitajika kwa ajili ya kudumisha afya bora na maendeleo ya binadamu.

Nchini Tanzania, Mpango huo unaangazia mazao makuu mawili ambayo ni mahindi yenye vitamini A na maharagwe yenye madini ya chuma. Ongezeko la ulaji wa mahindi na maharagwe yaliyoimarishwa kwa kuongezwa viini lishe, litasaidia kupambana na udumavu unaosababishwa na utapiamlo.

Mtaalamu huyo anabainisha kuwa ili kufikia azma hiyo, wahusika wakuu wa mnyororo wa thamani kama vile wakulima, wasindikaji, wakusanyaji, wasambazaji na jamii kwa ujumla, wanapaswa kutumia mbegu na vyakula vilivyorutubishwa kwa viini lishe.

Badala ya kutumia mahindi meupe na maharagwe ya kawaida yanayopatikana sokoni, hakuna budi kutumia mahindi na maharagwe lishe. Pia shule zinapaswa kuanza kuwalisha wanafunzi chakula chenye lishe bora ili kupunguza utapiamlo.

Mpango huu umeonyesha mafanikio makubwa kutokana na kazi iliyofanywa na wasindikaji na wauzaji bidhaa kama vile Afco Investment, Ruaha Millers na Makange Millers kwa kuleta sokoni vyakula vyenye virutubishi vingi na kuhakikisha wauzaji wa vyakula shuleni wanahama kutoka vyakula vya kawaida kwenda kwenye vyakula vyenye virutubisho na viini lishe.

Pamoja na kupata ushuhuda kutoka kwa wadau hao. Pia nilidodosa kidogo matumizi ya mbengu zilizofanyiwa biofortification kutoka Taasisi ya Udhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI). Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI, Patrick Ngediagi, alithibitisha kuwa mbegu zilizofanyiwa biofortification haikatazwi kisheria na zimebadilishwa kijenetiki (genetic modified seeds). Alikwenda mbali zaidi na kusema mbegu hizi zinadhibitiwa na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 pamoja na kanuni zake za 'Biosafety Regulations' za mwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2015.

Hivyo kwa uwapo wa utaalam huu wa biofortification kuongeza lishe kwenye vyakula vyetu, hakuna tena sababu ya nchi yetu kuendelea kuteshwa na utapiamlo na udumavu.

**Wasalaam.**
**Paskali**

**0754 270403**
**pascomayalla@gmail.comPascal Mayalla**

### MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Nani mwenye haki ya kuvunja sheria?



**Na Joseph Kulangwa**

**Mara ngapi katika barabara zetu hizi za mwendokasi hao hao madereva wetu wa Serikali wanaacha njia za kawaida na kuingilia njia za mabasi hayo ya mwendokasi, na hakuna anayewagusa, lakini wewe mwenzangu pangu pakavu tia mchuzi, uthubutu ukione.**

WASWAHILI bwana kwa semi hawawezekani. Mlishasikia semi mathalan, Mganga hajigangi; Kinyozi hajinyoi? Kama hujazisikia basi zipo na hutumika hata bila wakati mwingine mtumiaji kujua.

Kwamba unaweza ukawa na ujuzi fulani katika maisha yako lakini isikunufaishe wala kukusaidia chochote, matokeo yake unabaki na ujuzi wako mpaka unakufa nao.

Lakini wakati mwingine hutumika kumaanisha kuwa mtu hawezi kujiathiri au kujiumiza au kirahisi kuwa mtu hawezi kujiadhibu ila yuko mbele mbele kuadhibu wengine.

Tunashuhudia katika maisha yetu ya kawaida binadamu inakuwa rahisi kwake kuona kibanzi ndani ya jicho la mwenziwe lakini huku yeye akiwa na boriti jichoni mwake. Yaani makosa ya wengine anayakuza huku yake yakiwa makubwa zaidi.

Wako wale ambao hutumia usemi wa nyani haoni kundule. Maanake la mwenziwe analiona na pengine anaweza kulisema limekaa vibaya huku lake ndilo limejikalia kihasarahasara.

Jamii duniani huwa na sheria ambazo ni sharti zifuatwe. Na siku zote tunaambiwa katika jamii hakuna aliye juu ya sheria. Tukiambiwa pia kwamba hata rais hayuko juu ya sheria.

Lakini hebu kaeni mfikirie na kuwazua, ni kweli usemi huo una nafasi nchini? Sitaki niende juu kiuongozi ila nataka kuzungumzia tu watumishi wetu wa Serikali au wa umma, na mambo wanayoyafanya kwamba wako juu ya kila kitu.

Nazungumzia madereva wa Serikali wale wanaoendesha magari yetu yenye namba zinazoanza na ST, SU na hata hizi zenye namba za rangi nyekundu na nyeusi, lakini pia hata za balozi mbalimbali.

Unajiuliza hivi hawa watu wanajua kwa nchi hii ina sheria za barabarani kweli? Pengine wanatoka sayari nyingine! Utasikia kila kukicha wakuu wanaosimamia sheria za usalama barabarani, wanahanikiza kukemea matumizi mabaya ya barabara na uvunjaji sheria hizo.

Ni mara ngapi mathalan, ukifika katika njia kuu ambazo kuna mahali umeandikiwa 50, kwamba endesha gari lako eneo hili usivuke mwendokasi wa kilometa 50 kwa saa. Lakini madereva hao ni wa mwendokasi wa kuua mtu.

Mara ngapi katika barabara zetu hizi za mwendokasi hao hao madereva wetu wa Serikali wanaacha njia za kawaida na kuingilia njia za mabasi hayo ya mwendokasi, na hakuna anayewagusa, lakini wewe mwenzangu pangu pakavu tia mchuzi, uthubutu ukione.

Sasa inakuwa ina maana gani Serikali mathalan kukemea uvunjifu huo wa sheria hiyo, lakini watumishi walewale wanaotangaza sheria hizo ndio hao hao wanaopita kwenye njia hizo bila hata kuzuiwa?

Inaumiza zaidi pale ambapo unaona abiria katika magari hayo ni wakuu wa wilaya, ni wakuu wa mikoa, ni wakurugenzi, wakuu wa mashirika ya umma, mbaya zaidi ni mabosi wa Polisi ambao ndio wanaotakiwa kusimamia sheria hizo.

Kama itakuwa hivyo, kwamba anayetangaza marufuku ndiye huyo huyo anayeivunja marufuku hiyo, lakini raia akikosa amekosa, huku kiongozi akikosa hajakosa? Inatoa taswira gani kwa jamii?

Kupiga marufuku kitu au tabia fulani ni utaratibu wa maisha uliokubaliwa na jamii husika, hivyo ikitokea mtu akakiuka hata kama awe wa cheo, umri, rangi au kabila au dini fulani, hilo halikubaliki kabisa.

Tumeshatangaziwa hadharani, kwamba hiki kisifanyike ina maana ni sheria iliyotungwa na Bunge na kupitishwa na wabunge waliochaguliwa na sisi wananchi na hatimaye sheria kusainiwa na Rais na kuanza kutumika.

Sasa kama sheria hiyo inakiukwa na baadhi ya watu bila hatua kuchukuliwa, huku kundi lingine likiivunja linachukuliwa hatua. Tukisema kuna ubaguzi itauma au tukisema kuna upendeleo itang'ata?

Kama Taifa hili tuliamua liwe la amani na utulivu, upendo na mshikamano, basi tunachokubaliana kitekelezwe si huyu haguswi lakini yule anaguswa, huko ni kujenga matabaka ndani ya nchi.

Tulishakubaliana, hakuna magari yasiyo mabasi ya mwendokasi kupita kwenye njia za mabasi hayo, ili yaendelee kwenda haraka, hivyo asitokee mtu mwenye cheo chake serikalini, kudhani kuwa katazo hilo halimhusu. Tusimamie kwenye haki, tusimamie tuyokubaliana. Kazi Itaendelea.

**Alamsiki!**

SAFU

## KONA YA UKWELI

# Agizo la DC Temeke kifuta machinga jasho lina ukakasi



Na Thobias Mwanakatwe

MIONGONI mwa wakuu wa wilaya ninaowakubali kwa uchapa kazi ni pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo.

Jokate alihamishiwa katika wilaya ya Temeke akitoka wilaya ya Kisarewe mkoani Pwani katika mabadiliko yaliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, Juni, mwaka huu.

Hakuna asiyefahamu kuwa wilaya za mkoa wa Dar es Salaam zina changamoto nyingi kuziongoza hasa kutokana na kuwa na idadi kubwa ya watu tena wenye tabia tofauti na waliotoka katika mikoa mbalimbali kwa ajili ya kutafuta maisha.

Nimeona baadhi ya mikoa na wilaya suala la kuwahamisha wafanyabiashara wadogo, maarufu kama machinga, kama lilivyotolewa na serikali, watendaji wa halmashauri wanakiuka utaratibu. Yaani wanatumia mabavu zaidi badala ya ustaarabu katika kutekeleza jambo hilo.

Miongoni mwa wilaya ambazo katika baadhi ya maeneo utaratibu umekiukwa ni Wilaya ya Temeke mkoani Dar es Salaam.

Nimemsikia kwenye vyombo vya habari Oktoba 27, mwaka huu, DC Jokate naye akilaani kitendo kilichofanywa na watendaji wa halmashauri kuwabomolea vibanda machinga eneo la Tandika wakati kulikuwa na mazungumzo yanaendelea ili wahamishwe kwa utaratibu wa kistaarabu.

Mkuu huyo wa wilaya katika hali ya kuonyesha kuchukizwa na kitendo kilichofanywa na watendaji wa halmashauri dhidi ya machinga, alimwagiza Mkurugenzi wa Manispaa kuwapa kifuta jasho machinga wa Tandika.

Agizo hilo la DC ndilo limeibua hoja kwa nini malipo yawe kwa machinga wa Tandika tu wakati wilaya yake yote tukio hilo limefanyika?

Kama kuna malipo yoyote yale, ni wajibu wa waathirika wote wapatiwe kiasi hicho kulingana na athari zilizompata mhusika na siyo kuwagawa waathirika katika makundi.

Pia agizo hilo la mkuu wa wilaya linaibua swali lingine, je, malipo haya yanalipwa kwa tathimini ipi ambayo imefanyika au wanalipa tu holela? Nachofahamu utaratibu ni kwamba kama unatoa chochote lazima tathmini ifanyike kwanza ndipo malipo yafanyike.

Isije ikawa malipo haya yanafanyika kana kwamba kuanua jamvi juani tu, ili jamii nyingine ione kama kuna hisani imefanyika wakati kumbe ni danganya toto kula kunde mbichi.

Pia malipo aliyoyaagiza mkuu wa wilaya yanalipwa kutoka mfuko wa maafa au halmashauri husika? Kwa namna suala la machinga kama ilivyo ni maafa kwa wananchi basi kama kuna malipo yanapaswa kutoka katika mfuko wa maafa.

Kama agizo alilotoa huyu mkuu wa wilaya kuwa mkurugenzi mtendaji alipe pesa hizo maana yake pesa hiyo itatolewa katika mfuko wa halmashauri ya wilaya husika.

Kwa hiyo kamati ya mipango na fedha ya halmashauri lazima iketi kulijadili agizo hilo na DC naye DC atawakilishwa na Katibu Tawala wa Wilaya (DAS) wake maana yeye (DAS) ni mjumbe halali wa kikao hiki kama mkuu wa idara.

Kama fedha ipo katika mfuko wa halmashauri, ni fedha inayokusanywa kutoka vyanzo mbalimbali kutoka kila kata ya halmashauri hiyo. Kwa hiyo hoja ya kuwafuta jasho machinga wachache ni vigumu kupita kwa kuwa kila diwani katika kata yake kuna waathirika wa kubomolewa vibanda.

Suala hili linaibua hoja ya malipo kwa machinga nchi nzima katika kila pahala ambapo vibanda hivyo vimebomolewa, ili kuondoa maneno na malalamiko maana yake tathmini ifanyike na watu wote walipwe.

Kinyume chake, jambo hili si dogo kama linavyotazamwa ni jambo kubwa huku yule aliyeagiza machinga kuondolewa ndiye anayepaswa kulaumiwa zaidi.

Kama kila inavyogushwa kuna moto unaowaka suluhu ya suala hili ni kukaa kimya machinga warudi katika maeneo yao kama kawaida wafanye biashara yao kama mwanzo.

Katika ulimwengu wa biashara ni jambo la msingi ili mtu kuweka fedha yake katika biashara ahakikishiwe usalama wa mali hiyo na uhakika kwa biashara hiyo kufanyika bila bugudha yoyote.

Changamoto ya machinga inaweza ikatazamwa kwa jicho la kawaida kumbe hali hii ikafanya hata idadi ya maduka ilikuwepo ikapungua kuogopa na kuwa mashaka mengi.

Mathalani wizi wa kuanza kuvunja maduka unaweza ukarejea ambalo lilikuwa jambo la hatari miaka ya nyuma na kumbuka kuwa machinga waliondolewa wanatambua kuwa wanaondolewa kwa hoja ya wenye maduka.

Lakini pia kukosa kwao kufanya biashara kunaweza kukawavuta kushiriki vitendo vya kiarifu.

Mzigo huo wote watabebesha ndugu zetu polisi ambalo binafsi nasema siyo jambo zuri wala lenye tija kwa taifa letu ambalo kwa sasa linatimiza miaka 60.

Miaka 60 ya mingi ambayo kwa hakika kila linalofanyika liwe na ustarabu kwa kina na siyo kuamua bila ya kutazama madhara ya jambo hilo.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**mwanakatwe 2005@yahoo.com**

## DARASA LA NDOA

# NDOA SI TAASISI YA KUONGOZWA KWA UBABE



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

NI mpango asilia wa Mungu kwamba mume na mke waishi pamoja katika amani na utulivu kamili. Mume na mke katika ndoa wanategemeana. Mungu aliumba mwanamume na mwanamke ili wahitajiane na kutegemeana katika maisha. Pamoja na kwamba wajibu na majukumu yao hutofautiana, wana umuhimu sawa katika familia na jamii. Wote ni muhimu katika ustawi wa familia na jamii.

Maandiko Matakatifu ya Mungu yanaonyesha na kuainisha nafasi na wajibu wa baba na mama katika familia. Jukumu kubwa alilopewa baba ni kuwa kiongozi wa familia yake. Katika kutekeleza jukumu la uongozi, baba amepewa mamlaka na Mungu ya kuongoza familia yake kwa upendo na si kibabe. Uongozi wa kibabe ndani ya familia nyingi umebomoa badala ya kujenga. Umeondoa mvuto wa baba kwa familia yake na kufisha pendo la ndoa.

Mara nyingi uongozi wa kibabe humfanya mke ajisikie ni kiumbe duni asiye na thamani na mchango katika familia. Wanawake wengi wamepoteza hali yao ya kujiamini kwa sababu ya ubabe wa waume zao. Pamoja kwamba baba ni kiongozi wa familia, lakini hana budi kufahamu kuwa mafanikio katika kutekeleza majukumu yake ya uongozi katika familia yanategemea mke wake. Kwa hiyo, kujua kuishi na mke kwa akili ni jambo la busara.

Wanandoa wanahitaji umoja na mikakati ya pamoja ili kukabili changamoto na kufanikiwa katika maisha yao. Njia nzuri ya kushinda vita na maadui ni wanandoa kuishi kama timu moja yenye lengo na mwelekeo mmoja na si ubabe kwani ubabe huondoa hisia chanya za mke kwa mumewe.

Wanawake wanapenda sana kushirikishwa. Kwa kufanya hivyo, wanawake huongezewa hali ya kujiamini zaidi. Uongozi shirikishi katika familia una baraka nyingi kuliko uongozi wenye misingi ya ubinafsi. Ushirikishwaji unapokosekana huzaa migogoro ndani ya ndoa na sintofahamu nyingi.

Kinababa wanaotambua nafasi za wake zao katika familia, huwashirikisha katika uamuzi na usimamizi wa familia. Hata hivyo, mke akiona hashirikishwi inabidi ajitathmini na kumuuliza mume wake ili kujua sababu za kutokushirikishwa kwani inawezekana wakati mwingine tatizo liko kwa mwanamke mwenyewe. Mwanamke akijua tatizo ni vyema ajisahihishe ili ashikirishwe.

Kimsingi, mke anaposhirikishwa hujisikia kutambulika na kufanya vizuri zaidi. Hali hiyo humuongezea hisia za mapenzi, huvutiwa na mume wake na kutoa ushirikiano mzuri.Kinababa washirikishaji hufanikiwa sana katika maisha yao. Baba amtambue mke wake kuwa ni mwenzake mwenye mchango katika masuala ya familia na mwenye haki ya kushirikishwa. Mwanamke hujisikia fahari anaposhirikishwa mambo yanayohusu mustakabali wa familia yake.

Baba adumishe mawasiliano mazuri na mke wake kama ambavyo mke naye anapaswa kufanya hivyo kwa mume wake. Mawasiliano katika ndoa ni moja ya daraja linalounganisha wanandoa. Ni injini inayofanya ndoa iwe katika mwendo. Kumjua mwenzi kunaanzia na mawasiliano. Mume na mke wanapokuwa hawana mawasiliano mazuri kati yao, wanakosa kufahamiana vizuri, uhai katika uhusiano huondoka hivyo hudumaza pendo la ndoa. Mawasiliano mazuri yanapokuwapo heshima na thamani ya uhusiano wao huongezeka.

Baba kama kiongozi wa familia awe mfano mwema kwa kauli, mwenendo na matendo yake. Maisha ya baba na mkewe yawe mfano bora kwa watoto. Awe muadilifu na muwajibikaji katika familia. Baba asipowajibika katika familia yake anapoteza umuhimu na thamani ya uwepo wake.

Baba ajifunze kugawa madaraka yake. Kugawa madaraka ni jambo muhimu kwani si kila jambo lazima lifanywe na baba. Baba amtengenezee mazingira mke wake ya kujiamini na kubeba majukumu ya familia. Kuna mambo ya kufanywa na baba, mama, na mengine ya kufanywa na watoto. Baba anapotaka kufanya kila kitu mwenyewe anakaribisha msongo mkubwa wa mawazo, mgogoro na kifo cha mapema.

Mungu hakukusudia mume na mke waishi kwa mashindano bali kwa kukamilishana na kusaidiana. Kiongozi mzuri hujali vipawa na uwezo wa wale anaowaongoza. Hivyo, baba mwenye kujali hutambua vipawa, uwezo au udhaifu wa mke wake. Hivyo, humtia moyo na kumsaidia mke wake inavyopaswa badala ya kumhukumu na kuona hafai. Kwa ujumla, wanawake hupenda mwanamume anayejali hisia zao na maendeleo yao.

Kinababa wasiwe sababu ya kuleta upweke katika familia. Familia nyingi zimekosa kufurahia uwepo wa baba kwa sababu ya muda mwingi baba kutokupatikana nyumbani. Kina baba wengi wakiisha kuleta mahitaji ya nyumbani wanaona wamemaliza. Ni muhimu ikafahamika kuwa, kutunza familia ni zaidi ya kutoa mahitaji ya nyumbani. Familia inamhitaji baba kuliko vitu. Ukaribu wa baba kwa familia yake ni muhimu zaidi kuliko vitu. Wewe baba mwenzangu toa mahitaji lakini upatikane nyumbani pia.

Pamoja na majukumu mengi kinababa walio nayo ni muhimu kutengeneza muda wa kuwa na familia zao. Watoto wengi leo wana malezi ya mama zaidi kuliko baba. Jambo hili si zuri na lina gharama zake huko mbele ikiwa ni pamoja na baba kupuuzwa. Kazi zisiwe kisingizio cha kudumu cha kinababa kukosa muda na familia zao. Familia ni kitalu cha maisha yenye uto. Inapendeza na kutia moyo familia inapomfurahia baba na baba anapoifurahia familia yake.

**■ Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

MAISHA
NOVEMBA 7, 2021
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili




Ukurasa 14

**Onekana mjanja na Sneakers**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Vitu vya asili vinavyopendezesha nyumba



## HARUSI


Ukurasa 12



# Namna ya kuondoa sugu mikononi

Ukurasa 14

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA




HERUFI ZA MBUNI WANAOFANANA NI


**B & C**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | J | A | M | B | O |
| | A | | | A | |
| A | R | I | | K | |
| | I | | D | O | A |
| | B | | | R | |
| B | U | N | D | A | |


## AMSHA AKILI




| | |
|---|---|
| KITABU | |
| BARUA | |
| FUNGUO | |
| BEKI | |




## TOA TOFAUTI 5






## WATOTO

# PAKA RANGI



## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
ONA, IBA, BOMBA, PAMBA, BANANA, BEMBEA

## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma alikuwa na mama yake wakienda shambani, walipokuwa wakitembea Juma alikuwa nyuma ya mama yake akimfuata kwa taratibu. Walipokuwa wakikaribia shambani mama yake alimuuliza.

**Mama:** Mwanangu Juma Leo unaumwa?

**Juma:** Mama sina tatizo lolote, ila nimeamua kutembea nyuma yako

**Mama:** Wee mtoto umenitisha nilijua umeanza kupatwa na homa.

**Juma:** Hapana mama, ila mwalimu alituambia kwamba kutangulia si kufika.

**Mama:** Mwanangu huo ni msemo tu, mwalimu wako alimaanisha kwamba kufanya jambo kwa haraka huwezi kufanikiwa.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Unajua vita iliyoko kwenye nafasi yako?

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada zetu za Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki kadhaa nimezungumzia sana vyanzo vya migogoro katika maisha yetu, aina na jinsi ya kuitatua. Lakini kabla ya hapo nilikatisha mada kuhusu nafasi au cheo na vita inayotikisa maeneo hayo.***

LEO tuangalie vita kwenye nafasi yako. Ni vema ukaelewa kwamba nafasi yoyote unayoitaka kwenye ulimwengu wa damu na nyama lazima ianze kwenye ulimwengu wa roho (usioonekana). Usihangaike kutafuta nafasi yoyote ile, iwe ni kuoa au kuolewa kwenye ulimwengu wa damu na nyama hutaipata.

Nafasi yoyote nzuri unayotaka uipate kwenye ulimwengu huu wa kawaida ni lazima uanze kuipata kwenye ulimwengu wa roho. Kwa mfano, shetani aliposhindwa katika ile vita, maandiko yanasema, "wala mahali pake hapakuonekana tena mbinguni.

Shetani aliposhindwa, nafasi yake ilifutwa. Unaposhindwa vita vya kiroho, nafasi yako ya mafanikio inafutwa. Ndio maana wapo watu wanapambana, wanahangaika kupata nafasi fulani hawaipati siyo kwa sababu haipo, bali walishashindwa kwenye ulimwengu wa roho.

Hizo ndoto unazoota, ndio una nafasi nzuri, lakini unaota upo kijijini kwenu, maana yake tayari umeanza kushindwa kwenye ulimwengu wa roho. Una cheo, ni sawa, unafanya biashara nzuri ni kweli, wewe ni mtumishi wa Mungu una kiwango cha juu cha upako, lakini unapoanza kuota umerudi shuleni, au kijijini kwenu kule ulikozaliwa, ujue umeanza kushindwa kwenye ulimwengu wa roho.

Anza kutafuta nafasi kwenye ulimwengu wa roho. Na ukishaipata hata wakati kwenye ulimwengu wa kawaida, nafasi yako itakuwepo. Wapo watu huwezi kuwafukuza kazi, ukilazimisha utawarudisha mwenyewe.

Mtu mmoja akafukuzwa kazi akasema, "nakushukuru kwa kunifukuza kazi, nafuu nikapumzike". Kila ilipochukuliwa hatua kuiziba nafasi ile ilishindikana, ikabidi wamrudishe kwa aibu. Wapo watu hawafukuziki, huwezi kuwaondoa kwani hawaondoleki. Na wapo watu wanajijua kabisa kwamba nafasi zao haziwezi kuchukuliwa na wengine.

Wanadamu tunapaswa kumuomba sana Mungu atupatie kitu cha ziada kwenye nafasi zetu. Mungu huanza kukutengenezea nafasi kabla hujaipata. Hata kama upo kidato cha pili, Mungu tayari ameshatengeneza mume au mke wako.

Lazima uelewe kwamba nafasi yako itakuingiza kwenye vita. Unapoona vita ya aina fulani ujue una nafasi nzuri. Kama huna nafasi yoyote, basi huna vita yoyote. Ndio maana ni lazima ukubali kupambana kwa ajili ya nafasi yako. Lengo la adui ni kukutoa kwenye nafasi yako!

Nyoka aliwatoa wanadamu wa kwanza (Adamu na Hawa) kwenye nafasi kwa kuwapa tunda. Kwa hiyo, wapo watu walishaondolewa. Hata kama wapo, hiyo nafasi siyo halisi ni bandia lakini ile halisi haipo.

Yatupasa sana kumuomba Mungu aturudishie nafasi zetu tulizopoteza kwani yeye ni muweza wa vyote. Wapo viongozi walipoteza nafasi lakini akawarudishia. Na hata wali waliowasahau, wakawakumbuka tena. Nafasi inakupa heshima na pale unapoipoteza, marafiki hata ndugu hukupiga kisogo.

Hapa namaanisha kwamba ukiondolewa kwenye nafasi yako hakuna atakayekukumbuka. Mtu anaweza kuwa na cheo kikubwa lakini akifilisika tu, wale aliowasaidia hawamtafuti. Laiti watu wote uliowasaidia wangekutafuta wakakusaidia usingekuwa ombaomba. Ukishaondolewa kwenye nafasi yako ulimwengu wa roho, wale uliowasaidia wanakuona wewe ni mhalifu.

Ni kwa sababu kuna kitu cha kichawi kilifanyika kukuondoa kwenye nafasi ndio maana wale marafiki na uliowasaidia hawakukumbuki. Lakini baada ya kurudishiwa nafasi yako, utaona waliokusahau wanaanza kukutafuta.

Nafasi yako itafanya watu wakutafute, wakukumbuke. Mungu anapotaka kukurudisha kwenye nafasi yako, cha kwanza lazima fahamu zako zirudi. Maisha Ndivyo Yalivyo. Wapo watu ambao fahamu zao hazijarudi. Unaweza kujiona upo sawa kumbe siyo!

Mungu anapotaka kukurudisha kwenye nafasi, cha kwanza anashughulika na akili yako. Wapo watu hawana ile akili ya ki-Mungu. Hawana ufahamu wa kiroho na wanajiona wapo sawa kumbe siyo sawa kwenye akili ya Mungu. Labda upo sawa kwa kipimo cha majirani lakini siyo kipimo cha mbinguni.

Wapo watu huomba; Mungu naomba niinue, nirudishie nafasi lakini hawamtafuti kwa bidii wakidhani wanaweza kwa akili zao wenyewe. Muombe arudishe ufahamu uwe na akili ya kiroho ndipo atarudisha vyote.

***Hadi wiki ijayo, kwa maoni, kisa tuma ujumbe 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Suala la machinga lisiwe nguvu ya soda

SUALA la machinga bado limeendelea kuwa mjadala mkali huku kasi ya kuwaondoa kwenye maeneo wasiyostahili ikiendelea kiasi cha kupanga miji husika na kuifanya ionekane vyema tofauti na awali walivyokuwa wakifanya biashara kila mahali.

Kumekuwa na mitazamo tofauti kuhusu suala hili huku wengine wakipinga na wengine wakiunga mkono kwa kuwa hata nchi zilizoendelea haziachi machinga wakawapo kila mahali kila wakati.

Kwa hapa nchini, idadi ya machinga ilikuwa inaongezeka na bahati mbaya hawakuelezwa ukweli bali waliachwa waongeze vibanda kila mahali, kiasi kwamba kila ulipokamilika ujenzi wa barabara fulani basi vibanda vilipangwa juu ya mitaro ya maji ya mvua kama nyuki.

Kama haitoshi, kasi ya kujengwa vibanda vya mbao kwenye vituo vya daladala, kando ya barabara na mbele ya maduka ya biashara, iliongezeka kwa wingi kiasi cha wenye maduka kushindwa kufanya biashara.

Hata maeneo ya Posta na kwingine ambako haikuwahi kutarajiwa kuwa na vibanda vya machinga viliendelea kumea kwa kasi kubwa, huku kwenye vituo vya mabasi nako vikiongezeka.

Ni kweli wanatafuta maisha lakini ni lazima mji upangwe. Sheria na kanuni za mipango miji zinapaswa kufuatwa ndiyo maana zilitungwa kuliko kuendelea kusema waachwe watafute riziki huku mji ukionekana ovyo na kuzitukanisha sheria, kanuni na taratibu za miji na majiji.

Kwa sasa ukitembea Dar es Salaam unaona jinsi mji ulivyostahili kuwapo. Lakini unapozungumza na baadhi ya machinga, wanasema wako likizo fupi kwa kuwa suala hilo ni nguvu ya soda itafika wakati serikali itasahau nao wataanza kurudi kidogo kidogo.

Miaka ya nyuma jitihada kama hizi zilifanyika lakini ziligubikwa na siasa kwa kuwa wagombea walitumia suala la machinga kama mtaji wa kupata kura huku wakiendelea kuharibu miji na majiji.

Wako ambao walitoka kwenye kulipa kodi za serikali na kuwa machinga kwa kuwa hawalipi kodi wala tozo yoyote na wengine walikuwa na mtaji mkubwa ambao kimsingi wanapaswa kulipa. Pia wako waliokuwa na vibanda zaidi ya kimoja kisha wanakusanya mapato yao.

Kwa hali hiyo, aliyekuwa anaumia ni serikali kwa kisingizio cha machinga, sasa jitihada zimefanywa na wameondolewa na tayari serikali inakuja na suluhisho la kuhakikisha maeneo yanatengwa.

Ni kweli ni muhimu kuwatengea maeneo lakini lazima nchi ijitengeneze mazingira ya kuhakikisha hatuwi na machinga wengi, bali wafanyabiashara wengi wanaokuwa kila siku ili kuongeza walipa kodi na kupata fedha za kuendesha nchi.

Hakuna sababu ya mtu kuwa machinga miaka yote bali aonekane akikuwa na kuwa na biashara ya kati ambayo itatoa ajira ndogo na italipa kodi kwa serikali kuu.

Ni muhimu wanasiasa wakaacha kutafuta kiki kwa kuwa muda wa kuwadanganya watu ili kupata kura zao haupo bali ni wakati wa kujenga nchi kwa kuwaambia ukweli na kusimamia vyema sheria, mwisho watazoea na watalipa kodi.

Kuna watu wanajiita machinga, ukiangalia bidhaa walizonazo zikiingizwa kwenye duka dogo mtaani zinajaa, na kuna mtu amekuwa kuwa mwaminifu hataki kufanyabiashara barabarani amefungua duka analipa kodi zote muhimu alafu machinga anakuja anapanga bidhaa kama zake mbele yake.

Wanaotetea kuwa machinga wasiondolewe hebu wavae viatu vya wenye maduka Kariakoo ambao iliwapasa kugeuza kuwa stoo kwa kuwa machinga walijaa mbele ya maduka yao na kuuza bidhaa hizo hizo kwa bei ndogo sana kwa kuwa hawana gharama ya kodi ya pango na serikali wala ankra za umeme na maji.

Wanatoa mifano ya nchi zilizoendelea kama China kuwa zina machinga mtaani, ni kweli lakini siyo kweli kuwa wanaruhusiwa kuwa kila mahali, na la msingi lazima tujiulize uchumi wa nchi hiyo ndiyo uchumi wa Tanzania?

China ni nchi yenye uchumi mkubwa duniani kamwe hatuwezi kujilinganisha eti kwa kuwa wameacha machinga kwenye mitaa nasi tufanye hivyo, wanaoumia siyo viongozi bali wananchi wote ikiwamo machinga wenyewe.

Maumivu ni pale kodi inapopungua maana yake mgawo wa keki ya taifa utapungua badala ya kujenga zahanati, shule au kupeleka maji kwenye eneo A, huduma hizo hazitakuwepo.

Ni muhimu sasa serikali ikaendelea na mpango wa kufunganisha shughuli za kiuchumi na kuboresha huduma za kijamii maeneo yote nchini, kwamba mtu aweze kukaa kijijini au kwenye mji wake na kufanya biashara kuliko kuendelea kuwaambia kuwa mjini au jijini pekee ndiyo kuna maisha.

Kama miundombinu ya barabara na umeme itakuwepo ya kutosha, kama huduma nyingine muhimu za kijamii zitakuwapo hakuna sababu ya watu kukimbilia mjini na pia itakuza na kupanua miji midogo na baadaye maendeleo kusambaa hadi vijijini.

***Mungu ibariki Tanzania***

## HARUSI



Ulikuwa usiku wa kufurahi kwa ndugu na jamaa wa Beatrice Mushi katika hafla fupi ya kumuaga (sendoff), iliyofanyika Aprili 18, mwaka huu, katika ukumbi wa Buffalo, Mbezi Beach mkoani Dar es Salaam.









MITINDO







# Onekana mjanja na Sneakers

MIAKA iliyopita sneakers maarufu kama raba zilikuwa zinatumika zaidi kwenye kufanyia mazoezi lakini sasa mambo yamebadilika.

Sneakers zinaweza kuvaliwa kwenye 'outfit' na ukaonekana nadhifu.

Wakati wa majira ya joto, kama hivi sasa kwa nchi za magharibi, utagundua kwamba sneakers zimekuwa miongoni mwa vitu vinavyovaliwa zaidi hususani kwenye mitoko ya kawaida.

Wanawake nao wanashika hatamu siku hizi kwenye sneakers. Kwa wale wanaotamani kutoka wakiwa simple lakini stylish unaweza kujaribu kuvaa outfit na sneaker.

Wabunifu wa kampuni za raba kama Giuseppe, Adidas, Converse wako mstari wa mbele kutengeneza sneakers kwa ajili ya wanawake ambazo zinatumika kama vivazi nje ya mazoezi.

Unaweza kuvaa sneakers na aina nyingi za nguo kuanzia sketi, suruali za kitambaa, Jeans, kaptula na hata magauni ya maksi.

Kwa bongo, wadada wengi wanapenda kuvalia sneakers na magauni ya 'loose'.

Katika ulimwengu wa mavazi unatakiwa kwenda na dunia inavyokwenda na ukatolezea.



UREMBO



# Namna ya kuondoa sugu mikononi







NGOZI nyeusi katika magoti na nyuma ya mikono hutokana na mkusanyiko wa seli zilizokufa lakini pia unapoweka presha kwenye magoti na nyuma ya mikono yako.

Ukiwa unaweka mikono kwenye meza ukiwa kazini, ule msuguano unafanya ngozi iwe nyeusi hasa kwenye kisugudi.

Hata hivyo, huna haja ya kuwa na hofu kwa sababu unaweza kutumia njia hizi za asili kuondoa weusi huo:

**JUISI YA ALOE VERA**

Juisi ya Aloe Vera inasaidia kuondoa weusi. Unachotakiwa kufanya ni kupaka juisi hiyo kwenye sehemu yenye weusi na uache kwa nusu saa kisha unawe mikono na upake moisturiser. Rudia kufanya hivi angalau mara mbili kila siku.

**BINZARI, MANJANO, ASALI NA MAZIWA**

Changanya vyote hivi ambapo matokeo ni mchanganyiko mzito. Paka kwenye magoti na kwenye mikono yako palipo na weusi.

Kaa nao kwa nusu saa. Nawa na paka moisturiser. Rudia kufanya hivi kila siku kwa wiki kati ya tatu na nne, Bila shaka utapata matokeo mazuri.

**NDIMU**

Chukua pamba na uitumie kupaka juisi ya ndimu katika sehemu zenye weusi. Au unaweza kuikata ndimu na kuipaka kwenye sehemu unapotaka kuondoa weusi. Kaa nayo kwa muda wa saa moja kisha nawa. Rudia hivi kila siku hadi weusi utakapopotea.

**MAFUTA YA MIZEITUNI NA SUKARI**

Changanya vizuri, hii itakuwa kama scrub kwa ajili ya magoti na mikono.

Paka hizo sehemu zenye weusi kisha unamasaji polepole. Nawa kwa maji ya fufutende kisha paka moisturiser.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Salad yenye nyama ya kuoka







SALAD ni chakula bora na wengi wetu tunapenda kula salad kama chakula ili kuzuia kuongeza uzito.

Mapishi haya yanaonyesha jinsi ya kuongeza vionjo kwenye salad kwa kula na nyama ya kuoka.

Nyama ya iliyookwa ni afya na nzuri zaidi kula kwa kiasi na kwa hamu.

**MAHITAJI**

Nyama ya ng'ombe nusu kilo unaweza pia kutumia mbuzi au aina tofauti, karoti mbili kata vipande vidogo, tangawizi moja imenywe na kusagwa.

Vitunguu saumu viwili vilivyosagwa, pilipili hoho mbili, kijani na nyekundu zilizokatwa, kitunguu maji kikubwa kimoja kikatwe vipande vidogo na Salad.

Nyanya mbili, pilipili manga, Olive Oil, limao moja lililokamuliwa, Tango moja,

**NAMNA YA KUANDAA**

Pasha moto oven kwenye nyuzi joto sentigredi 250 na acha iwe ya moto kwa muda wa dakika tano hadi 10.

Andaa nyama, kata vipande wastani, osha kisha weka kwenye bakuli ya kioo au chombo unachotumia kupikia kwenye oven.

Ongeza viungo, kitunguu saumu, tangawizi, pilipili manga. Changanya vizuri.

Weka chumvi, changanya vizuri, kamulia limao, kisha changanya vizuri mchanganyiko.

Menya viazi, kata vipande, changanya kwenye nyama, weka karoti, pilipili hoho, kitunguu maji na changanya vizuri, weka olive oil, changanya vizuri.

Weka mchanganyiko wa nyama na viungo kwenye oven, weka muda dakika 40 na angalia mara kwa mara kama nyama inaiva vizuri au inaungua na geuza ili kuifanya iive kwa uwiano mzuri.

**OSHA SALADI YAKO VIZURI**

Weka kwenye chombo kikubwa, kata kwenye vipande vidogo kwa kutumia mikono, kata nyanya, tango kwenye vipande vidogo, changanya salad, nyanya na tango.

Mlo wako utakuwa tayari kwa ajili ya kuliwa kama mlo wa usiku itapendeza zaidi.

MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



## Vitu vya asili vinavyopendezesha nyumba



MANDHARI ya nyumba inapendeza kutokana na ubunifu na uhitaji wa MTU husika. Wapo wanaopendezesha nyumba zao kwa vitu mbalimbali ambavyo vinawekwa ndani au nje. Katika kupeana maarifa kuhusu upambaji wa nyumba, hizi ni baadhi ya dondoo za namna ya kupamba nyuma kwa vitu vya asili.

**1:** Unaweza kupamba nyumba yako kwa kutumia ngozi halisi za wanyama. Aina hii ya mapambo inafaa kuwekwa sebuleni, varandani au chumba cha chakula.

**2:** Tumia vibuyu kupamba nyumba yako. Aina hii ya mapambo inapendeza sehemu tofauti ya nyumba, hakikisha vibuyu vinakuwa na michoro tofauti ili kumfanya mtu kuvutiwa nayo.

**3:** Ungo na vitu vya aina hiyo ni pambo zuri ndani ya nyumba. Weka ukutani ungo za aina na rangi tofauti na matokeo yake utayaona.

**4:** Mitungi ya asili pamoja na kuwa sehemu nzuri ya kuhifadhi maji, pia inapendezesha mwonekano wa nyumba pale inapowekwa ndani. Hakikisha unanunua mtungi wenye rangi nzuri na wenye michoro ya kuvutia.

# Vijue vipaumbele vya nyumba yako unapokutana na mtaalamu

NI ukweli usio na shaka kuwa kila mtu anahitaji kuwa na nyumba bora, safi na salama kwa matumizi mbalimbali ikiwamo makazi na biashara.

Pamoja na utofauti wetu wa kipato, bado ni baadhi tu ya Watanzania wenye hamasa ya kuwa na nyumba bora za kisasa zitakazowafanya kufurahia juhudi zao katika kuifanya furaha kuwa sehemu ya maisha.

Mazingira safi na salama ni matokeo chanya ya kuwa na makazi bora na salama, thamani ya maisha yako ni nyumba, fahari ya nyumba ni upekee wake katika kuifanya dunia kuwa sehemu bora na salama kwa maisha yako.

Ubunifu wa aina tofauti wa nyumba zinazoendelea kujengwa sehemu mbalimbali zimekuwa kivutio kikubwa kwa watu ndani ya jamii na kuchangia kwa kasi ukuaji wa miji na vijiji nchini ambayo pia yanatokana na matokeo chanya ya kuwa na wataalamu bora na wenye weledi katika fani ya ubunifu, usanifu na usimamizi wa ujenzi.

Pamoja na mabadiliko yanayoendelea kutokea, bado kuna baadhi ya watu hawajafahamu vizuri hatua mbalimbali katika kuwafikia wataalamu watakaowasaidia kutimiza malengo ya kumiliki nyumba bora za kisasa.

Hata hivyo, nimeona leo tuzungumzie vitu muhimu vinavyopaswa kuulizwa, kushauriwa na kuelewa pale unapokutana na mtaalam wako wa kukujengea nyumba. Kwa kushirikiana na mtaalam wa masuala ya ujenzi, Peter Msuya, atatuelezea zaidi vitu muhimu vya kuhoji unapokutana na mtaalam wa kufanya kazi yako hiyo.



Msuya anasema moja ya mambo ya kuhoji ni mwonekano gani unataka nyumba yako iwe kwa kuzingatia ubora.

Anasema wataalamu wa ujenzi ni watu wanaozingatia sana mwonekano bora wa nyumba wakati wa ubunifu na wakati wa ujenzi, hivyo unapohoji ni rahisi kufahamu aina ya nyumba wanayokujengea.


Msuya anasema unapaswa kuwa na utambuzi kwenye ufahamu wako aina gani ya nyumba unayohitaji ikiwamo kuwasilisha vizuri mapendekezo yako ya aina nyumba ambayo wewe unaamini kuwa utaipenda na itakufaa kwa matumizi yako uliyokusudia.

Kwa mujibu wa Msuya, vyovyote utakavyomweleza na kuuliza kuhusu mwonekano wa namna nyumba yako itakavyoonekana, mtaalamu wako ana uwezo mkubwa wa kufanya chochote kwa kuzingatia mambo mbalimbali ya kitaaluma na kwamba yapo mambo mengi yanayomuongoza katika utendaji wa kazi yake.

Ushiriki wako, anasema ni muhimu sana kwa kuwa kuna baadhi ya mambo yanahitaji ushiriki wa karibu sana wa kimajadiliano katika uboreshaji wa ramani za nyumba wakati wa ubunifu.

"Yako mambo unayoweza kuyapenda wewe lakini kwa wengine ni chukizo, ni kawaida sana hayo kutokea lakini ni muhimu kusikiliza maoni ya wengine yatakayo kusaidia kuboresha baadhi ya upungufu ambao hukuuona na mwisho mtaalamu wako ndiye atakayekusaidia kuboresha mwonekano bora wa nyumba yako," anasema Msuya.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
UKOSEFU WA AJIRA
BONGOFLEVA
SINGELI
TUTABANANA HUKU HUKU!!!
BAR GANI AMBAYO MPAKA SASA HATUJAKOPA ILI TUKASOMESHE TUACHE DENI KAMA TUNAVYOACHA KWINGINEKO?
NIMEWASHA DATA 'GOOGLE' INASACHI BADALA YA KUNASA BAR INANASA 'RB' TUNAZOTAFUTIWA
ZOEZI LA KUSOMBA WAMACHINGA... NIMECHUNGULIA SERO NIMEKUTANA USO KWA USO NA MWANANGU WA KUFIKIA!
MI MWENZAKO KATIKA ZILE VURUGU 'NIMEMKOGESHA' MIRUNGU BA'MKWE BILA KUJUA! SIJUI KAMA NDOA YANGU BADO IPO!
MANKA! WE MWANAMKE HAYO MAPENZI GANI JAMANIIIII? UTANIUA PUMZI INAKATA...
KILA SIKU UNANIIJIA NA KANENO KAKO ETI "AILAFIYUU!" UNASANI NIMETOKA MOSHI KUJA DARESALAMA KUSIKILISA MANENO?
WE MWANAUME GANI? TOKA UNIOE RAHA NAZIONA KWA MAJIRANI TU KATIKA NDOA ZAO!...LAKINI WEWE SIJAWAHI KUPATA RAHA KWAKO!
EMBU NIKUMBUSHE HUENDA NIMESAHAU ...KWANI NILIPOKUOA NILIKUAHIDI NAKU-PELEKA 'PEPONI?'
MGANGA NIPIGIE RAMLI MAANA MWENZAKO SIJIELEWI
MIMI NI 'DOKTA' SIO MGANGA... PIA SIPIGI RAMLI BALI MIMI NAPIGA "YUTRASAUNDI" USINTAFUTIE JELA BWEGE WEWE!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...NAFUU INAGHARAMA KUBWA

# Mlipuko wa lori la mafuta waua zaidi ya 90 Sierra Lione

**FREETOWN,** SIERRA LEONE

WATU 91 wamefariki dunia na wengine kadhaa kujeruhiwa baada ya kutokea mlipuko katika Mji Mkuu wa Sierra Leone, Freetown.

Mlipuko huo ulitokea siku ya Ijumaa, baada ya lori la mafuta lenye urefu wa futi 40 kugongana na gari lingine kwenye makutano jijini humo.

Picha za video zilizorushwa na vyombo vya habari vya ndani zilionyesha miili iliyoungua vibaya.

Hadi sasa hakuna idadi kamili ya vifo, wakati katika chumba cha kuhifadhia maiti kinachosimamiwa na serikali tayari kimepokea miili 91. Kwa mujibu wa meneja wake, aliyeliambia Shirika la Habari la Reuters.

Rais wa Sierra Leone, Julius Maada Bio, alisema amesikitishwa na moto huo mbaya na vifo vya kutisha vya watu.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter, alisema, serikali yake itafanya kila kitu kusaidia familia zilizoathirika.

Meya wa Freetown Yvonne Aki-Sawyerr alieleza kuwa aliona picha "za kutisha" lakini ukubwa wa athari za tukio hilo hazijafahamika.

Kupitia ukurasa wake wa Facebook alisema, "Kulikuwa na uvumi kwamba zaidi ya watu 100 wamepoteza maisha,"

Mlipuko huo unaaminika ulitokea kwenye makutano nje ya Duka Kuu la Choitram lililo na shughuli nyingi katika eneo la Wellington mjini.

Mkuu wa Shirika la Kitaifa la Kukabiliana na Majanga la Sierre Leone, Brima Bureh Sesay, aliviambia vyombo vya habari kuwa tukio hilo lilikuwa "ajali mbaya". Mwezi Machi, mwaka huu tukio kama hilo lilitokea nchini humo na kuwaacha zaidi ya watu 80 wakiwa wamejeruhiwa kwa moto na huku 5,000 wakiwa hawana makazi.

Na mwaka 2017 zaidi ya watu 1,000 walipoteza maisha baada ya mvua kubwa kunyesha na kusababisha maporomoko ya matope yaliyokumba jiji hilo na kuwaacha karibu watu 3,000 bila makazi.

**BBC**



Makundi tisa yanayoipinga serikali ya Ethiopia kikiwamo Chama cha Tigray People's Liberation Front, yamekubali kuunda muungano dhidi ya utawala wa Waziri Mkuu Abiy Ahmed. **BBC**

## Wapiganaji wa Tigray na makundi mengine yaunda muungano

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

VIKOSI vya wapiganaji wa jimbo la Tigray na makundi mengine ya upinzani nchini Ethiopia, vimetangaza kuungana dhidi ya serikali ya Waziri Mkuu, Abey Ahmed, kwa lengo la kushinikiza kipindi cha mpito baada ya mwaka mmoja wa vita.

Muungano huo mpya unajumuisha wapiganaji wa jimbo la Tigray, kundi la wapiganaji kutoka jamii ya Oromo na makundi mengine saba yanayopambana na vikosi vya serikali ya shirikisho nchini Ethiopia.

Ushirikiano huo umetangazwa wakati ripoti zinasema wapiganaji wa Tigray wanasonga mbele kuelekea Mji Mkuu Addis Abbaba, licha ya miito ya kusitishwa mapigano inayotolewa na Jumuiya ya Kimataifa.

Juzi Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwa mara ya kwanza lilitoa tamko la kutaka kukomeshwa kwa mzozo nchini Ethiopia na kuondolewa vizuizi vya kufikishwa msaada wa kiutu kwenye Mkoa wa Tigray unaoshuhudia uhaba mkubwa wa chakula.

**DW**

## Wanaharakati wa Mazingira kuandamana tena Glasgow

**GLASGOW,** SCOTLAND

MAANDAMANO zaidi yameendelea jana mjini Glasgow, unakofanyika Mkutano Mkuu wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi wa COP26, kwa lengo la kupaza sauti dhidi ya kile wanaharakati wa mazingira wanakitaja kuwa mwendo wa polepole katika kushughulikia ongezeko la joto duniani.

Wanaharakati wa mazingira akiwamo, Greta Thunberg, wamevunjwa moyo na majadiliano ya COP26, baada ya ripoti ya hivi karibuni kuonyesha kuwa utoaji wa gesi ya Kaboni unapanda kuelekea viwango vya kabla ya janga la Corona.

Licha ya mataifa kutoa ahadi ya kupunguza uchafuzi kama ilivyoafikiwa kwenye mkataba wa Paris, serikali nyingi duniani bado zinajivuta vuta kuachana na matumizi ya nishati chafuzi.

**DW**

## Marekani yatangaza donge nono kuwapata walanguzi wa dawa za kulevya

**WOSHINGTON D.C,** MAREKANI

SERIKALI ya Marekani imetangaza dau la hadi dola milioni tano kwa yeyote mwenye taarifa zitakazowezesha kukamatwa au kutiwa hatiani kwa raia wanne wa Mexico wanaotuhumiwa kwa ulanguzi wa dawa za kulevya.

Miongoni mwa hao wanne ni Aureliano Guzman-Loera ambaye ni kaka wa Joaquin "El Chapo" aliyetiwa hatiani na kufungwa jela mwaka 2019 kwa kuingiza mamilioni ya kilogramu za dawa za kulevya nchini Marekani chini ya genge la uhalifu liitwalo Sinaloa.

Wizara ya sheria ya Marekani imesema pia inatafuta taarifa za ndugu watatu wa familia ya Nevarez ambao wanafanya kazi chini ya mwavuli wa kundi la Sinaloa linaloendesha mtandao mkubwa wa usafirishaji dawa za kulevya duniani.

Miongoni mwa makosa yanayowakabili ni kuingiza dawa aina ya fentanyl ambayo kati ya mwaka 2020 hadi 2021 inahusishwa na asilimia 63 ya vifo vya matumizi yaliyopindukia ya dawa za kulevya nchini Marekani.

**DW**

## MAKALA

# MAADILI YA VIONGOZI KUELEKEA MIAKA 60 YA UHURU, TUKO WAPI?



Na Magabilo Masambu

JULAI 7, 1963 katika sherehe za kitaifa za Sikukuu ya Sabasaba, kusherekea kuzaliwa kwa TANU mwaka 1954, Baba wa Taifa, mwalimu Julius Nyerere, akihutubia umma wa Watanganyika alisema: "Nalazimika kusema waziwazi kuhusu jambo ambalo nimekuwa nikililalamikia kwa muda sasa. Nalo ni tabia inayokua ndani ya serikali kuchanganya kati ya utu na ufahari." (Uhuru na Umoja uk. 223).

Haya yalisemwa miaka michache tu tangu uhuru wa Tanganyika na baadaye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baada tu ya uhuru, baadhi ya viongozi ndani ya serikali wakaanza kuyatumia madaraka kuonyesha ufahari kama ambavyo leo karibu miaka 60 ya uhuru baadhi pia wanayatumia vibaya.

Lakini miaka michache baadaye, yaani mwaka 1967, Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya TANU iliyokutana katika ukumbi wa mikutano Arusha Januari 26 mpaka 29, ikatangaza Azimio la Arusha, ambalo wengi waliliita azimio la misingi ya utu. Azimio la Arusha lilikuwa na mambo mawili makubwa. Mosi, utaifishaji wa njia kuu na nyeti za uchumi na pili, utungwaji wa miiko ya uongozi wa serikali, mashirika ya umma na chama (Simulizi za Azimio la Arusha, 2017).

Muda mfupi baadaye, manung'uniko ya viongozi yakaanza chinichini serikalini hasa kuhusu miiko ya uongozi. Miezi miwili tu baada ya kupitishwa kwa Azimio la Arusha, Mzee Rashidi Mfaume Kawawa aliwatangazia wabunge kwamba kama wana maswali juu ya Azimio wayawasilishe na yatajibiwa. Katika kuitikia wito huo, yaliwasilishwa takribani maswali 21 ambayo yalijibiwa na Mwalimu Nyerere mwenyewe.

Hapa kuna fundisho kubwa sana la kiuongozi kwamba kama watu wana malalamiko juu ya mambo fulani, mnawaruhusu wayaseme waziwazi na faida yake ni kwamba mtajua ama mlipokosea au walipokosea wao. Tabia za viongozi leo kutumia nguvu kubwa kuzima manung'uniko na maoni ya watu, imekuwa kubwa hasa Afrika. Hii nafikiri inaweza kuwa sababu ya mapinduzi tunayoyashuhudia yakiendelea katika ukanda huu, maana kama watu hawana mahala pa kusemea waende wapi.

Bahati mbaya tu maswali yote yaliyo wasilishwa yalihusu sehemu moja tu ya Azimio, yaani miiko ya uongozi. Hapakuwa na swali lolote lililohusu ujamaa na kujitegemea lakini bado mwalimu aliyajibu pamoja na kwamba yalikuwa yanapinga mawazo yake juu ya ujamaa. Hii inaonyesha kwamba miiko ya uongozi iliwabana sana viongozi kutoyatumia vibaya madaraka yao.

Jambo jili liliendelea kuwa na upinzani mkubwa kiasi kwamba baadaye yaliibuka maazimio mengine, ambayo Mwalimu aliyaita maazimio yalioua Azimio la Arusha bila viongozi kutamka waziwazi na kuna wakati alifika mahala, anasema ili kuzungumzia dhana ya ujamaa na kujitegemea inakubidi uwe kama mwendawazimu lakini mpaka anaaga dunia aliendelea kuamini katika misingi ya ujamaa na kujitegemea pamoja na miiko ya viongozi.

Leo tunalalamika kuhusu maadili ya viongozi lakini kwa ujanja tuliipinga miiko ya uongozi yenyewe. Pengine busara ilikuwa kufanya marekebisho kwa baadhi lakini ikaendelea kutumika kwa baadhi ya mambo ili kuepusha hali ilivyo leo ambapo uongozi unaonekana kama sehemu ya kuonyesha ufahari, kuwa na mali zisizoelezeka na mengine kadhaa yanayofanana na hayo.

Kama alivyosema Waziri Mkuu Kassim Mjaliwa kuhusu baadhi viongozi wa umma kuwa na walinzi binafsi (mabaunsa) na kuonyesha kuchukizwa na tabia hiyo, jambo kama hilo linapigwa marufuku na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 132(1). Maana yake kama tuna viongozi wanaovunja Katiba hawastahili kuwa ofisini labda jambo kama hilo lifanyike kwa sababu maalum.

Katika eneo linalolalamikiwa zaidi katika uvunjifu wa maadili ni vijana wanaopata fursa za kuwa viongozi, hawa wengi wanabebwa na ujana, ulimbukeni, ushamba na kudhani kwamba wao ndio wamekuwa viongozi wa kwanza katika nchi hii. Huwa nasema ukiwa mkuu wa wilaya unapoingia ofisini, jambo la kwanza omba orodha ya wakuu wa wilaya ofisini kwako ili uone kumbe wewe si wa kwanza, walishakuwapo kitambo na hata ofisi zingine fanya hivyo hivyo.

Bahati mbaya tulionayo sasa ni kuamini wenye elimu kubwa kama sifa mama ya mtu kuchaguliwa kuwa kiongozi. Ni kweli elimu zao zinawasaidia kuzipata nafasi hizo, lakini tabia zao zinaamua ni kwa muda gani watadumu na nafasi hizo. Ni wakati sasa mtu ili awe kiongozi, asitazamwe tu kwamba ana digirii ngapi za chuo kikuu maana mtu kama si mwadilifu hata digirii anaweza kuwa amenunua.

Ushauri wangu kwa vijana kuelekea miaka 60 ya uhuru, ukipewa madaraka umepewa nafasi nzuri ya kujenga uhusiano na watu, umepata nafasi ya kujenga kesho yako ya siasa na uongozi, vitisho na majivuno havina nafasi katika kutengeneza kesho yako.

Kila wakati jifunze kwa waliokutangulia hata kwa mambo unayoyajua. Huko nyuma hatukuwa tunaaminika kumbe inawezekana wazee walitufahamu tuondoe mtazamo huo kwa kujishusha badala ya kupandisha mabega. Habari ya kwamba ujana ni maji ya moto, lazima tujue vilevile kuwa maji ya moto huwa hayaunguzi nyumba ya majani.

Nikijibu swali langu kwamba tuko wapi sasa, nafikiri tumerudi nyuma badala ya kwenda mbele. Kama tutasema waliotutangulia walifanya na wanafanya vizuri katika nyanja ya uongozi kimaadili, maana yake huko mbele tutakuwa na hatari zaidi kwa sababu wenye maadili wanapungua na wajinga wanaongezeka.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Solemba na Libeneke zilivyozalisha msamiati



Na Adam Fungamwango

MUZIKI una kazi kubwa sana duniani ya kuelimisha, kuburudisha, kuonya na hata kufikisha ujumbe kwa njia mbalimbali. Ujumbe wa muziki hufika vizuri na hukaa kwenye vichwa vya watu zaidi kuliko ukitolewa kwa njia nyingine kama hotuba na risala.

Rais wa Awamu wa Nne, Jakaya Kikwete, alishawahi kusema msanii au mwanamuziki hufikisha ujumbe kwa wananchi na kueleweka kwa urahisi zaidi kuliko hata mwanasiasa. Ni kweli kabisa, maana kuna wakati hata taifa hasa miaka ya nyuma ilitegemea wanamuziki watunge nyimbo kwa ajili ya kuelimisha wananchi, kuwatia moyo, kuwaonya na mengine yanayofanana na hayo.

Mfano wakati wa ukombozi Kusini mwa Afrika, nchini kama Msumbiji, Namibia, Afrika Kusini na Zimbabwe ambazo zilikuwa hazijapata uhuru, wanamuziki wa Tanzania walitumika kutunga nyimbo za kuhamasisha ukombozi, hali ambayo ilitia chachu kwa wapiganaji na viongozi ambao wengi wao walikuwa wakiishi hapa nchini, chini ya Mwenyekiti wa uliokuwa Umoja wa Nchi Tano Zilizo Mstari wa Mbele kwa Ukombozi wa Kusini mwa Afrika, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Wakati vita ya kumtwanga Nduli Idd Amini, wanamuziki wa Kitanzania walipishana studio kutunga nyimbo ambazo ziliwatia moyo wananchi pia kuwaondolea woga, hadi nchi iliposhinda vita hivyo mwaka 1979.

Mbaraka Mwinshehe alitunga nyimbo za kuelimisha juu ya ulaji wa chakula bora na akavitaja vyakula vyenyewe, kiasi kwamba hata mtu hasubiri kuambiwa na daktari, au kusoma kwenye vitabu, akiukariri tu wimbo huo, anajua chakula gani anachotakiwa kula na kina kazi gani mwilini. Wimbo mwingine ulikuwa wa kuhamasisha wananchi kuweka pesa zao benki na kueleza faida zake na athari za kuzifukia nyumbani.

Hii ndiyo kazi ya muziki, ingawa kwa kizazi cha sasa chenyewe kimejikiza kwa zaidi ya asilimia 90 kwenye mapenzi. Tena kikitumia maneno yasiyo ya staha.

Wanamuziki wa zamani walishawahi kutunga nyimbo ambazo zimeumba misamiati ambayo ilikuwa ikizungumzwa mitaani kwa wakati huo, lakini kuna misamiati mingine imeendelea kudumu hadi leo hii. Hata vijana wa sasa wameirithi na wanaendelea kuitumia ingawa hawajui chanzo cha maneno hayo.

Tunaanza na wimbo wa 'Hanifa' wa Marijani Rajab. Kwenye wimbo huu unaozumzungia mwanamke mmoja aliyemwacha mumewe na kuhadaika na wanaume wa nje kiasi cha kukosa huku na huku, kuna kipande marejeni anaimba "Eee bwana huna (huna), hakutaki tena ee, baba na mama, na mume mwanangu huna."

Hilo neno 'huna' lilitengeneza msamiati mmoja ambao ulikuwa maarufu sana katikati ya miaka ya 1970 hadi mwanzoni mwa 1980. Mwanamke kama hamtaki mwanamume anayemwomba urafiki kwa namna yoyote ile, iwe hamtaki tu au hata pesa, basi atamjibu 'huna'. Neno hilo peke yake lilitosha kumpa ujumbe mwanamume kuwa hatakiwi.

Muhidini Gurumo, alipojiunga tu na Mlimani Park Orchestra, alitunga vibao viwili vilivyoondokea kuwa maarufu 'Kassim' na 'Kassim Amefilisika'. Wenyewe wanaviita Kassim namba moja na namba mbili. Cha kwanza ni cha mwaka 1978 na cha pili mwaka 1979.

Nyimbo hizi ziliunda misamiti miwili iliyokuwa maarufu miaka hiyo. Mtu ambaye ni mlevi kiasi kwamba anaisahau hadi familia yake, au inateseka kwa sababu ya ulevi wake aliitwa Kassim, hata kama jina lake ni Juma. Kuna kipande ambacho Gurumo anaimba "Unapotoka kazini unapitia kwenye baa, unapokuta marafiki, ukiagiza moja moto moja baridi."

Wakati ule sasa mtu akikwambia nakwenda kupata moja moto moja baridi. Hata hutaki ufafanuzi. Unajua kabisa anakwenda baa kunywa. Misamiati ilitokana na nyimbo za dansi ipo mingi, lakini kuna hii ambayo hadi leo inatumika.

Utasikia hata sasa mtu anakwambia "Jamaa anaendeleza libeneke" akiwa na maana anaendelea kitu ambacho amekianza. Au tabia ambayo anayo. Iwe nzuri au mbaya.

Wengi hawajui libeneke hiyo ni nini. Msamiati huu umetokana na wimbo wa Butiama Jazz Band chini ya Mzee Mkwenga na Alfonce Makelo unaoitwa 'Mtindo Libeneke'. Libeneke ni mtindo wa bendi hiyo kama ilivyo Msondo Ngoma au Sikinde Ngoma ya Ukae. Libeneke ni ngoma moja ya kienyeji Ifakara.

Kwenye wimbo huo, wanatajana majina wanamuziki wote wa bendi hiyo, na kuna kipande wanaimba "Waache waseme watachoka wao sisi tupo tunaendeleza libeneke." Wakiwa na maana wanaendeleza bendi yao yenye mtindo huo. Ndipo ulipozaliwa msamiati wa 'Kuendeleza libeneke."

Msondo Ngoma walitoa wimbo wa 'Solemba' katikati ya miaka ya 1980, uliotungwa na mwimbaji mlemavu wa macho, Nico Zengekala. Unaelezea jinsi alivyoahidiana na msichana aende kwao, lakini alipofika hakumkaribisha, jamaa alibaki nje huku solemba akichungulia dirishani tu.

Mpaka sasa hivi, hata vijana wanatumia msamiati huo. Yoyote anayedanganywa au kuambiwa wakutane sehemu fulani, halafu mwingine hakwenda, basi itatamkwa tu kuwa "Ameachwa solemba."

# HADITHI

# Ajenda ya siri-3

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je, ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**




MZEE alimgeuka mkewe na kumsihi waingie kwenye gari. Msichana yeye alionekana yuko tayari tangu mwanzo. Tatizo lilikuwa na wazee wake.

Baada ya kimya cha dakika 10, Eddy aliitafuna lami. Aliamua kuvunja ukimya.

"Mzee huyu mama ni mkeo?"

"Ndiyo ni mke wangu."

"Na huyu binti yako?"

"Sawa kabisa."

"Aliyehukumiwa na huyu nani mkubwa?"

"Hilo swali anayeweza kujibu ni mke wangu."

"Lakini naona kama hayupo vizuri kabisa."

"Atajitahidi, eti mama Mwasi, umesikia swali la huyu kijana?"

"Baba nikwambie tu, yule sio mwanangu wa kumzaa, ndiyo maana kama ulikuwepo mahakamani ulisikia akiniita shangazi."

"Ni mtoto wa kaka yako?"

"Hapana, yule alikuwa mfanyakazi wangu. Wakati anatoka kwao Mpanda, alipofika mjini alifikia kwangu. Kwa historia yake ni kwamba baba na mama yake walifariki zamani, akiwa mdogo. Kusema kweli jambo hilo lilinifanya kuishi naye sio kama mfanyakazi, bali ni kama binti yangu wa kumzaa na hata kazi kwa marehemu Chilambo alipata akiwa kwangu na alitoka kwangu. Kwanza nilikataa kabisa kumruhusu, roho yangu ilikuwa nyeusii, leo hii Tina anakwenda kunyongwa, siamini." Mama Mwasi akaanza kulia tena.

Ilibidi binti yake aanze kumbembeleza. Eddy alikuwa na kazi ya kubadili gia, huku akielekezwa sehemu wanayopaswa kupita na mzee yule.

"Mimi naitwa Eddy Kamal, kama nilivyowaeleza ni wakili, mzee ukaitwa nani?"

"Naitwa Digalu Pazi."

"Mama kashindwa kuendelea kunipa historia ya binti yule, wewe unaweza kunieleza kidogo?"

"Kaka alivyokwambia mama yako. Miaka mitatu iliyopita alikuja kwangu huyu binti akiwa ameongozana na msichana mwingine wa jirani. Alikuwa akitafuta kazi za ndani. Mke wangu hakuwa sana anahitaji dada wa kazi, msichana yule alikuja amechoka, anaonekana ametoka safari ndefu ana njaa, akataka kwanza akae, ale, apumzike. Baada ya kupumzika, akamhadithia historia yote ya maisha yake, alipotoka, madhila aliyokutana nayo alipotoka kwao, hadi kufika hapa. Na hapa alikuwa hana ndugu." Digalu aliendelea kumpa historia ya msichana Tina aliyehukumiwa kunyongwa.

**"Hapana kusema kweli. Unajua mimi mwanzo nilikuwa napingana na mke wangu kuhusu kumchukua mtoto wa mtu ambaye hatujui ametoka wapi, ndugu zake ni nani na ana tabia gani, lakini baada miezi mitatu tu, nadhani nilimpenda zaidi kuliko hata mke wangu kwa tabia zake, hata alikokwenda kufanya kazi, sifa zilikuwa zikimiminika, sasa sijui nini kilichotokea."**

"Mke wangu ni mtu wa huruma, baada ya kusikia historia yake kuwa alifiwa na wazazi wake, aliteswa na ndugu zake, shida alizozipata, akaona akimwambia hapa hakuna kazi, atakuwa kama ameemzidishia chumvi kwenye kidonda. Akaamua kumwambia akae pale, lakini kazi kubwa ilikuwa ni kumsaidia mke wangu kupika vitumbua, chapati, supu, chai na uji asubuhi."

Kabla hajaendelea zaidi, sauti ya mkewe ilisikika nyuma ya gari.

"Baba, nimeishi naye vizuri tu Tina, hata pale mtaani watu walimpenda. Ni mcheshi na uwepo wake yeye nilikuwa nikipata wateja wengi sana. Na hata kwenye maisha ya kawaida sasa, nilimfanya kama binti yangu wa kumzaa."

"Ikawaje tena mama akaenda kwa Chilambo?" Swali lilitoka kwa Eddy.

"Unajua tena baba, sifa zinafika mbali. Wateja hawa hawa walitapanya sifa, zikamfikia mke wa marehemu Chilambo ambaye alikuwa anataka mdada wa kazi. Mfanyakazi wake mmoja alikuwa ni mteja wangu wa supu ndiyo kaenda kumwambia. Tena alikuja na gari hadi nyumbani. Akanibembeleza, akaniambia atakuwa ananilipa mshahara kila mwisho wa mwezi na pesa zingine atakuwa ananiletea mimi nje ya mshahara, ndiyo nikakubali. Nikatafuta msichana mwingine wa kunisaidia yeye, akaenda huko Tegeta."

"Mama unaitwa nani?"

"Mimi mama Mwasi au jina langu ni Mtupeni."

"Mwasi ndiyo huyu binti yako si ndiyo?"

"Ndiyo?"

"Tina alikaa kwako kwa muda gani?"

"Miaka miwili."

"Hakuna lolote baya au lisilo la kawaida hata moja ambalo ameshawahi kufanya?"

"Kwa kweli baba hapana. Yule mtoto nimekwambia pamoja na kwamba alifiwa na wazazi wake akiwa mdogo, lakini ana nidhamu, heshima, hana makuu, hana makundi, kazi zote anajua na halalamiki. Yaani sijui nisemeje."

"Kule kwa Chilambo alifanya kwa muda gani?"

"Mwaka sasa."

"Eti mzee Digalu, umeshawahi kuletewa kesi au mlalamiko yoyote ya msichana yule?"

"Hapana kusema kweli. Unajua mimi mwanzo nilikuwa napingana na mke wangu kuhusu kumchukua mtoto wa mtu ambaye hatujui ametoka wapi, ndugu zake ni nani na ana tabia gani, lakini baada miezi mitatu tu, nadhani nilimpenda zaidi kuliko hata mke wangu kwa tabia zake, hata alikokwenda kufanya kazi, sifa zilikuwa zikimiminika, sasa sijui nini kilichotokea."

"Kwa nini msichana ambaye sifa zake ni nzuri, halafu amefanya tukio kubwa kama hili?"

"Baba, hata sisi tuko kwenye mshangao. Hatujui huko ilikuwaje." Alijibu mama Mwasi.

"Kuna tetesi kuwa alipewa au aliahidiwa pesa na baadhi ya wafanyabiashara aliokuwa wakigombana nao marehemu."

"Sijawahi kumuona na pesa zingine zaidi ya zile alizokuwa akilipwa. Kama angekuwa na pesa zaidi mimi ningejua. Labda wawe wamemdanganya watampa, halafu hawajampa."

"Unaamini kweli Tina amemuua Chilambo kwa kumuwekea sumu kwenye chakula?"

"Baba, mahakama imeshasema, sasa mtu kama mimi nitasema nini tena. Ila inaniuma, halafu sielewi, hivi kweli Tina nayemjua mimi? Labda kwa sababu moyo wa mtu ni kichaka."

"Pia kuna dhana alikuwa hajalipwa mshahara miezi sita, ni kweli?"

"Si kweli." Swali hili alijibu mzee Digalu.

"Pesa zake za kila mwezi alinipa mimi nimuwekee, zingine nilimwambia afungue akaunti benki aweke, kwa hilo hapana."

"Zingine nilikuwa nalipwa mimi, si nilikwambia na mimi nilikuwa napewa kama kifuta jasho kutokana na kuwapa msichana wangu. Tulikuwa tunalipwa kila mwezi." Mama Mwasi alidakia.

Tayari gari lilikuwa limeshafika maeneo ya Tandale kwa Mtogole. Alichofanya Eddy ni kuhakikisha anaifahamu nyumba ya mzee Digalu.

INAENDELEA JUMAPILI



# Q BOY MSAFI AVURUGWA NA MACHAWA

MSANII Q Boy Msafi ameibuka na kuwaambia wale wote wanaofanya kazi ya 'uchawa' kuwa wanapoteza muda na watajutia maisha yao baadaye.

Akasema kuwa kazi ya uchawa inasababisha mtu kuchelewa kufanya maisha yake ya baadaye na wanapoteza muda mrefu kushambulia mtu mwingine.

"Kama wao wanaona ni kazi sawa, lakini haina malipo ya baadaye. Malipo yake ni ya papo kwa hapo, na chawa wanapewa zaidi sifa kuliko pesa," anasema Q Boy, ambaye alitamba na ngoma za 'Achimwene', 'Yeye', 'Kongoro', 'Unaanzaje' 'Karirero' na nyingine nyingi.

Anasema kuwa hata Mungu alisema mwanamume atakula kwa jasho lake, hivyo inatakiwa kutengeneza ukubwa na ufahamu na kujituma ili kupata kipato bila kumtegemea mtu.

"Mimi hizo chembechembe sina, uchawa ni kukataa maisha yako na kumpa mtu mwingine alifanyie maisha yako," alisema.

Kwa sasa kumekuwa na watu ambao wanaitwa 'machawa'. Hawa hawana tofauti kubwa na wapambe. Ni watu ambao wanafanya kazi ya kupamba, kuwasifia na kuwatetea watu fulani, au mastaa kwa ajili ya kutengenezea sifa, umaarufu, lakini pia kuwalinda kwa maneno na wale ambao wanawachafua.

Baadhi ya wasanii nchini wamekuwa wakiwamiliki watu wa aina hiyo, ambao kwa sasa wanajulikana kwa jina la 'machawa'

## Muno apiga hodi Bongo

OVIEMUNO Oriero, maarufu kama Muno, amepanga kufanya ziara yake Afrika Mashariki, ikiwamo Tanzania.

Habari kutoka Nigeria zinasema, msanii na mwandishi kutoka Nigeria, anatarajia kutua kwenye jiji la raha na karaha, Dar es Salaam, au Bandari ya Salama mwezi ujao, Desemba.

Muno tayari amesharekodi ngoma kibao, ameshawahi kuwa chini ya label nyingi nchini Nigeria ikiwemo Lebo ya msanii Rude boy wa P Square inayoitwa "Rude Boy Records".



Wakati yupo Rude Boy Records, aliachia ngoma kama "Never regret" na baadae kushirikishwa kwenye ngoma ya "slow slow" ya Rude boy.

Kwa sasa yupo chini ya Management ya Champion on Entertainment LTD , ambapo ametoa Ep yake mpya inaitwa 4+1 ambayo iliachiwa September 17 mwaka huu 2021.

## Harmonize: Bando lenu, ila potezeeni

MSANII Hamornize amewaonya mashabiki wake wasijisumbue hata chembe kuweka bando lao, kuliharibu, kupoteza pesa zao kwa ajili ya kumpigia kura kwenye tuzo yoyote nje ya nchi.

Kwenye insta stori yake, Konde Boy, ameonyesha kutokukubalia na uteuzi wake, kuna mmoja wa wasanii wanaowania tuzo za AEAUSA, na AFRAMA.



"Nawaonya mashabiki wangu msijisumbue kuweka bando lenu na kuliharibu, kwani sijatajwa kwenye tuzo yoyote." aliandika msanii huyo maarufu nchini.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RUDIGER KUTUA MADRID

REAL Madrid wanatarajia kumsajili mlinzi wa kati wa Chelsea, Antonio Rudiger, 28, kwa uhamisho huru mara mkataba wake na klabu hiyo utakapomazika mwishoni ma msimu huu, na wanaweza kumpa Mjerumani huyo mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki. ***(AS,via Mail)***

### STEGEN ANUKIA NEWCASTLE

GOLIKIPA wa Barcelona, Marc-Andre ter Stegen, 29, ni kipaumbele cha usajili wa Newcastle United. ***(El Nacional)***

### VLAHOVIC KITAELEWEKA

MAOFISA wa Arsenal na Fiorentina walikutana jijini London wiki hii kujadili ofa itakayomfanya mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21 kuungana na washika bunduki hao. ***(Express)***

### POGBA ALIITEGA UNITED

KIUNGO wa Ufaransa, Paul Pogba, aliijulisha Manchester United mwaka 2019 kuwa atakuwa tayari kusaini mkataba mpya na klabu hiyo, lakini klabu hiyo iliamua vinginevyo. Mkataba wa mchezaji huyo utakamilika majira yajayo ya joto. ***(Mail)***

### CONTE AMTAKA BROZOVIC

KOCHA mpya wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte, anataka kumsajili mchezaji wake wa zamani, kiungo wa Inter Milan, Marcelo Brozovic, 28. Mchezaji huyo anatarajiwa kumaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu huu. ***(Tuttomercato)***

### CHELSEA YAMFUATA SZALAI

CHELSEA inataka kumsajili mlinzi wa Timu ya Taifa ya Hungary anayekipiga katika klabu ya Fenerbahce, Attila Szalai, 23. ***(Sun)***

### DE JONG MAMBO MAGUMU

BARCELONA watataka kukatiza mkataba wa mkopo wa mshambuliaji wa Uholanzi, Luuk de Jong, 31, kutoka Sevilla Januari. ***(Sport)***

### XAVI KUANZA NA COMAN

KOCHA mpya wa Barca, Xavi anataka kumfanya winga wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Kingsley Coman, 25, kuwa usajili wake wa kwanza. ***(Sport)***

### JOVIV KUONDOKA MADRID

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Serbia, Luka Jovic, 23, anashinikiza kuondoka Real Madrid katika dirisha dogo la Januari. ***(Defensa Central)***


### SILVA KICHEKO CITY

KIUNGO wa kati wa Ureno, Bernardo Silva, 27, alihusishwa kuondoka Manchester City majira ya joto, lakini amesema "anafuraha sasa" klabuni hapo. ***(Sky Sports)***

### KLOPP AMTAKA BOWEN

MSHAMBULIAJI wa West Ham, Jarrod Bowen, 24, amehusishwa na Liverpool na kocha wa klabu hiyo, Jurgen Klopp amekiri anavutiwa na mchezaji huyo. ***(Liverpool Echo)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# HATIMAYE XAVI RASMI BARCELONA

**Anatarajiwa kukabidhiwa mikoba ya Koeman leo huku mabosi wake...**

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA itamtangaza Xavi kuwa kocha wao mpya wa timu yao hapo kesho Jumatatu, kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Hispania.

**Gwiji huyo mwenye umri wa miaka 41 alitumia miaka miwili kama kocha wa Al-Sadd, lakini maofisa wa Barca walifikia makubaliano na klabu hiyo ya nchini Qatar ili kumrudisha Camp Nou.**

Miamba hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, wana matumaini Xavi ataijenga upya timu hiyo na kurudi kwenye zama zake baada ya kumtimua, Ronald Koeman.

Ikithibitisha imefikia makubaliano na Xavi, Barca iliweka taarifa yake kwenye Twitter ikisema: "Ilikuwa lazima iwe hivyo. Karibu nyumbani."

Na taarifa kupitia kwenye tovuti ya klabu hiyo iliongeza: "Barcelona imefikia makubaliano na Xavi kwa yeye kuwa kocha mpya wa kikosi cha kwanza kwa kipindi chote cha msimu kilichobaki na misimu mingine miwili zaidi.

"Xavi, ni zao la akademi ya vijana pale Barca, ameondoka Al-Sadd ya Qatar baada ya mazungumzo yaliyofanyika kwa siku chache.

"Inatarajiwa Xavi atawasili hapa Barcelona wikendi hii na Jumatatu tutamtangaza kuwa kocha mpya wa kikosi cha kwanza cha Barcelona na tukio hilo litafanyika kwenye Uwanja wa Camp Nou.


"Baada ya tukio la kumtangaza tutafanya mkutano na waandishi wa habari. Na tutaelezea kwa ufupi ajenda yetu kwa kumleta Xavi kuwa kocha wa kikosi cha kwanza."

Xavi anarudi Barca kuchukua mikoba ya ukocha baada ya kuondoka miaka sita iliyopita akiwa mchezaji.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwaka 2010, alibeba mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na tisa ya LaLiga kwa kipindi chote alichokaa na Blaugrana hao.

MECHI KALI
HOME
AWAY
WEST HAM
4.20 | 4.20 | 1.71
LIVERPOOL
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa
CHEZA USHINDE KASINO

# WAKALA WA POGBA AMSHUTUMU SOLSKJAER



**MANCHESTER,** England

WAKALA wa Paul Pogba, Mino Raiola, amemshutumu Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, kuwa ndio chanzo cha kiwango kibovu cha mteja wake msimu huu.

Pogba alianza msimu kwa kasi kwa kufanya usaidizi wa mabao saba katika mechi nne za mwanzoni mwa msimu huu wa Ligi Kuu England, lakini hali imekuwa tofauti hasa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya amekuwa hana kiwango bora kama hapo awali.

Raiola ameyasema hayo ikiwa mezani kwake kuna mkataba mpya kutoka Manchester United tangu Julai, mwaka huu ili kuongeza muda wa Pogba kusalia Old Trafford.

Taarifa mbalimbali zinaarifu Pogba amemtaarifu Raiola anafikiria kurejea Italia katika jiji la Turin ili kujiunga na wababe wa Serie A, Juventus ambako alicheza kwa miaka minne kabla ya kurejea United.

Hata hivyo, Pogba pia amekuwa akitajwa kuwaniwa na klabu kadhaa kubwa za Ulaya wakati mkataba wake na Mashetani Wekundu hao ukimalizika mwishoni mwa msimu huu.



# Firmino nje wiki nne

**LIVERPOOL,** England

STRAIKA wa Liverpool, Roberto Firmino atakosekana kwa wiki nne kwenye kikosi cha timu hiyo kutokana na majeruhi ya misuli aliyonayo.

Firmino mwenye umri wa miaka 30 ameifungia Liverpool mabao manne katika michezo nane ya Ligi Kuu England msimu huu na alipata majeraha hayo kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Atletico Madrid ambayo iliisha kwa Liverpool kushinda mabao 2-0.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp, akizungumzia kumpoteza nyota huyo amesema: "Tunazungumzia majuma, bado tuna zaidi ya wiki nne, nayachukulia ni majeraha makubwa."

Pia Klopp alizungumzia kuhusu kumwacha kiungo wake, Curtis Jones na mlinzi, Joe Gomez, kwenye mchezo watakaosafiri kwenda jijini London kuminyana na West Ham, leo Jumapili.

"Curtis ni habari nyingine tofauti na Firmino, yeye hakuwa na bahati mazoezini, yeye alipata majeraha kutokana na kidole kukwangua sehemu ya jicho, yeye yupo karibu kurudi ila itabidi tusubiri ni lini atarejea.

"Curtis, atarudi baada ya mapumziko ya kupisha michezo ya kimataifa, lakini baada ya michezo ya kimataifa tutaangalia ni lini anaweza kuwa sawa kucheza tena na Joe natumai naye atarudi baada ya michezo ya kimataifa pia."




# MBEYA KWANZA SASA YASUKA MASTRAIKA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mbeya Kwanza FC, Haruna Harerimana, amesema kazi kubwa anayofanya katika kikosi chake kwa sasa ni kuimarisha safu ya ushambuliaji ili iweze kupata mabao katika kipindi cha kwanza kwenye mechi za Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara ambayo wanashiriki.

Akizungumza na gazeti hili jana, Harerimana alisema amebaini tatizo la washambuliaji wake kushindwa kufunga katika mechi tano walizocheza na anatumia muda huu wa mapumziko kumaliza tatizo.

**Kocha huyo amesema wachezaji wake wanaonekana kukosa nguvu ya kufunga katika kipindi cha pili na kuruhusu wapinzani wao kusawazisha mabao ambayo wao wamefungwa.**

"Tuna wastani mzuri katika ligi kuu kwa kuanza vyema lakini bado kuna upungufu wa kufanyia kazi ikiwamo kuhakikisha tunaimarisha idara ya ushambuliaji, tunataka tuwe tunatumia ipasavyo nafasi tunazotengeneza hasa katika kipindi cha kwanza, ukiangalia katika mechi tulizocheza tunakuja kusawazisha katika kipindi cha pili, tunahitaji kuongeza umakini," alisema Harerimana.

Aliongeza pia ameendelea kuimarisha wachezaji wake katika safu ya kiungo kuwapa mbinu za kiufundi nyingine zitakazowasaidia kukabiliana vizuri na washambuliaji wa timu pinzani.

" Msimu huu ligi imekuwa ya ushindani mkubwa, ila ninaamini tunahitaji kupata matokeo mazuri katika mechi za mzunguko wa kwanza ili kujikusanyia pointi ambazo zitatuweka katika mazingira salama kwenye msimamo," kocha huyo aliongeza.



Watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Zanzibar, walioshiriki katika mbio za marathon zilizofanyika kwenye Uwanja wa Amaan jana katika maadhimisho ya mwaka mmoja wa Uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi. **PICHA: TRA**

# JKU FC matumaini ikiivaa Jang'ombe

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya JKU imedhamiria kuondoka na pointi tatu muhimu katika mechi yake ya Ligi Kuu ya PBZ Zanzibar dhidi ya Taifa Jang'ombe itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan Visiwani hapa.

JKU yenye pointi sita inashuka dimbani ikiwa ndio vinara wa ligi hiyo baada ya kushinda michezo yake miwili iliyopita huku Taifa Jang'ombe ikiwa katika nafasi ya 11 baada ya kutoka sare mara mbili.

Kocha Mkuu wa JKU, Sheha Mohamed, alisema anatarajia mchezo huo dhidi ya Taifa Jang'ombe utakuwa mgumu na ili kupata ushindi amepanga kutumia mbinu tofauti na zile zilizozoeleka.

"Timu ya Taifa Jang'ombe tunaiheshimu, ni timu nzuri na ina hamasa kubwa kutoka kwa mashabiki wake, kwa hamasa hiyo lolote linaweza kutokea uwanjani," alisema.

Naye Kocha wa Taifa Jang'ombe, Omar Khamis 'Matu' aliliambia gazeti hili matokeo waliyopata katika mechi zilizopita yamewajenga na yuko tayari kwa mchezo wa leo.

"Kutoka sare katika michezo miwili iliyopita inaashiria kikosi changu kipo imara, kila timu tunayocheza nayo inatukamia, lakini hatuna wasiwasi, tutapambana," alisema Matu.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Mau itakuwa ni kati ya KMKM dhidi ya Mafunzo wakati Mlandege itavaana na Uhamiaji huku Selem View ikiwakaribisha Zimamoto na Malindi watakutana na Polisi.

SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA




MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 07 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 2645 | Keciorengucu vs Genclerbirligi | 2.05 | 3.32 | 3.22 |
| 14:00 | 1754 | Ural Yekaterinburg vs Zenit St Petersburg | 9.29 | 5.33 | 1.27 |
| 14:30 | 2720 | Venezia vs Roma | 5.60 | 4.30 | 1.54 |
| 15:00 | 5765 | Dundee FC vs Celtic | 9.68 | 5.53 | 1.26 |
| 15:15 | 4800 | Sheffield Wed vs Plymouth | 1.97 | 3.56 | 3.51 |
| 15:30 | 1287 | Brugge vs Standard Liege | 1.29 | 5.51 | 8.47 |
| 16:00 | 2478 | Oxford Utd vs Bristol Rovers | 1.65 | 3.95 | 4.64 |
| 16:00 | 2484 | Vejle BK vs Sonderjyske | 2.24 | 3.44 | 2.95 |
| 16:00 | 3271 | Fatih Karagumruk vs Galatasaray | 3.15 | 3.49 | 2.12 |
| 16:00 | 5302 | Asteras Tripolis vs Lamia | 1.78 | 3.31 | 4.74 |
| 16:00 | 5602 | Villarreal vs Getafe | 1.52 | 3.94 | 6.79 |
| 16:30 | 3667 | Rostov vs Rubin Kazan | 2.43 | 3.10 | 2.90 |
| 16:30 | 4323 | Fortuna Sittard vs PSV Eindhoven | 8.65 | 5.70 | 1.27 |
| 17:00 | 1198 | Lorient vs Brest | 2.43 | 3.24 | 2.89 |
| 17:00 | 1386 | Everton vs Tottenham | 3.01 | 3.21 | 2.41 |
| 17:00 | 2448 | Tondela vs Maritimo | 2.21 | 3.22 | 3.22 |
| 17:00 | 2554 | Reims vs Monaco | 3.82 | 3.42 | 1.96 |
| 17:00 | 2568 | Udinese vs Sassuolo | 2.38 | 3.46 | 2.86 |
| 17:00 | 3203 | St Etienne vs Clermont Foot | 2.47 | 3.33 | 2.78 |
| 17:00 | 3746 | Leeds vs Leicester | 2.71 | 3.51 | 2.47 |
| 17:00 | 3797 | Sampdoria vs Bologna | 2.36 | 3.50 | 2.85 |
| 17:00 | 4609 | Arsenal vs Watford | 1.44 | 4.68 | 6.55 |
| 17:00 | 5153 | Nantes vs Strasbourg | 2.39 | 3.19 | 2.99 |
| 17:30 | 1624 | Hertha BSC vs Bayer Leverkusen | 3.38 | 3.53 | 2.06 |
| 18:00 | 1167 | Bolton vs Stockport | 1.60 | 4.14 | 4.83 |
| 18:00 | 1957 | Rochdale vs Notts County | 1.78 | 3.84 | 3.94 |
| 18:00 | 2295 | Kolos Kovalivka vs Shakhtar Donetsk | 11.58 | 5.41 | 1.21 |
| 18:00 | 3543 | RFC Seraing vs KAA Gent | 5.12 | 4.23 | 1.55 |
| 18:15 | 1574 | Valencia vs Atletico Madrid | 4.00 | 3.35 | 1.95 |
| 18:15 | 3649 | Volos vs Aris Salonica | 3.25 | 3.20 | 2.20 |
| 19:00 | 2507 | Fenerbahce vs Kayserispor | 1.47 | 4.44 | 5.92 |
| 19:00 | 3949 | Nice vs Montpellier | 1.56 | 4.30 | 5.20 |
| 19:00 | 4436 | Kocaelispor vs Bursaspor | 2.25 | 3.37 | 2.79 |
| 19:30 | 2534 | West Ham vs Liverpool | 4.20 | 4.20 | 1.71 |
| 19:30 | 2918 | FC Koln vs Union Berlin | 2.08 | 3.52 | 3.32 |
| 20:00 | 1420 | Hapoel Hadera vs Nazareth Ilit | 1.98 | 3.23 | 3.52 |
| 20:00 | 1915 | Lazio vs Salernitana | 1.33 | 5.42 | 8.24 |
| 20:00 | 1971 | Napoli vs Verona | 1.40 | 4.91 | 7.01 |
| 20:00 | 3152 | Santa Clara vs Porto | 6.90 | 4.44 | 1.42 |
| 20:00 | 5431 | Sparta Prague vs Teplice | 1.13 | 8.16 | 17.91 |
| 20:30 | 2489 | Royal Antwerp vs Anderlecht | 3.16 | 3.60 | 2.08 |
| 20:30 | 3337 | Panathinaikos vs PAOK | 2.85 | 3.19 | 2.44 |
| 20:30 | 4381 | Osasuna vs Real Sociedad | 3.05 | 3.20 | 2.38 |
| 20:30 | 5345 | Mallorca vs Elche | 2.05 | 3.11 | 4.01 |
| 20:30 | 5858 | Olympiakos vs Ionikos Nikea FC | 1.14 | 7.27 | 16.70 |
| 21:30 | 5595 | Greuther Furth vs Eintracht Frankfurt | 3.59 | 3.69 | 1.94 |
| 21:45 | 2823 | Maccabi Tel Aviv vs Hapoel Tel Aviv | 1.81 | 3.47 | 3.85 |
| 22:45 | 1074 | Rennes vs Lyon | 2.58 | 3.53 | 2.53 |
| 22:45 | 3009 | AC Milan vs Inter | 3.04 | 3.54 | 2.23 |
| 23:00 | 1135 | Betis vs Sevilla FC | 2.79 | 3.24 | 2.54 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Novemba 7, 2021

Nipashe



Hatimaye Xavi rasmi Barca UKURASA 21




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kulia), akimvisha medali mshindi wa kwanza wa mbio za kilomita 21 za Zanzibar Blue Economy Half Maradhon 2021, Natalia, baada ya kuibuka kidedea katika mbio hizo zilizofanyika Visiwani humo, jana. **PICHA: IKULU**

## Samatta, Msuva watua kunogesha Taifa Stars

**Na Saada Akida**

NAHODHA wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta na mshambuliaji, Simon Msuva, watawasili nchini kesho kwa ajili ya kujiunga na timu hiyo inayojiandaa na mechi ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), imefahamika.

Taifa Stars inayonolewa na Kim Poulsen, raia wa Denmark itaikaribisha DRC katika mchezo wa marudiano wa Kundi J utakaochezwa Novemba 11, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Meneja wa Taifa Stars, Nadir Haroub 'Cannavaro', alisema jana tayari Novatus Dismas anayecheza soka la kulipwa katika klabu ya Maccabi Tel Aviv ya Israel ameshajiunga na wachezaji wenzake kwenye kambi hiyo ambayo inaendelea na mazoezi hapa jijini.

"Tumeona upungufu wetu katika mechi yetu dhidi ya Benin na tunaufanyia kazi, hatutaki kurudia makosa tuliyofanya katika mechi hiyo ambayo tulipoteza tukiwa nyumbani mara tutakapowavaa DRC," Cannavaro alisema.

Aliongeza mikakati iliyopo ni kuhakikisha ushindi unapatikana katika mechi hiyo na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kuwafuata Madagascar baada ya siku chache.

"Wachezaji walioko kambini wako fiti na molari ya hali ya juu, tunatarajia kupambana kutafuta matokeo mazuri ya ushindi ili kujiweka katika nafasi ya kuendelea kuongoza kundi letu," alisema Cannavaro.

Stars yenye pointi saba sawa na Benin wanaongoza katika Kundi J wakifuatiwa na DRC yenye pointi tano wakati Madagascar wakishika mkia wakiwa na pointi tatu mkononi.

# Yanga yamtaka Chama

### ●●● Simba yenyewe yawatuliza mashabiki na kutamba ubingwa Ligi Kuu Bara...

**Na Saada Akida**

WAKATI uongozi wa Simba ukisema mikakati yao ya kuhakikisha wanatetea ubingwa wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara msimu huu imeimarika, mabosi wa Yanga wameweka wazi wanahitaji huduma ya kiungo wa kimataifa kutoka Zambia, Clatous Chama.

**Simba pia ndio mabingwa wa mashindano ya Kombe la FA na baada ya kutolewa kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, sasa watakutana na Red Arrows ya Zambia kwenye mchezo wa hatua ya mtoano katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.**

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again', alisema klabu imeweka mipango yake vizuri katika kuhakikisha wanafanya vizuri katika ligi pamoja na mashindano ya kimataifa ambayo wanashiriki ili kuendelea kujenga heshima.

Salim alisema hawatarudia makosa yaliyojitokeza kwenye mechi ya marudiano dhidi ya Jwaneng Galaxy na sasa 'wameamka' kuhakikisha bendera ya Msimbazi inapepea vyema.

Alisema tayari wameshaanza maandalizi kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting ambao utachezwa Novemba 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza na unaofuata dhidi ya Reds Arrows utakaofanyika mwishoni wa mwezi.

"Dhamira ya Simba siku moja ni kushinda ubingwa wa Afrika, bado nia iko pale pale, tunaimani hiyo siku itafika, mashabiki watulie Simba ipo imara itatetea ubingwa na kufanya vizuri kwenye Kombe la Shirikisho Afrika," alisema Salim.

Aliongeza ili kufikia malengo, wachezaji wanatakiwa kujituma na kupambana katika kila mechi na kwa kufanya hivyo, hawatapoteza dira huku akiweka wazi dirisha dogo la usajili litakapofungiliwa, 'panga' linaweza kuwapitia baadhi ya nyota.

"Hapo hatutaangalia jina la mchezaji, ambaye hatakuwa tayari kuisaidia klabu ataachwa bila kujali ameifanyia nini Simba," Salim alisema.

Alisema kwa sasa timu yao inapita kwenye 'upepo mbaya', lakini anaamini kitakaa sawa na kurejea katika makali yaliyozoeleka.

"Ninawaambia Wanamsimbazi wasikate tamaa juu ya timu yao kutokana na namna ilivyo kwa sasa, hiki ni kipindi cha mpito na wafahamu ligi ndio kwanza imeanza, mambo mazuri yanakuja mbele, watulie," Salim alisisitiza.

Naye Mjumbe wa Kamati ya Mashindano ya Yanga, Hersi Said, aliliambia gazeti hili timu yao inatamani kumpata Chama kwa sababu ni moja ya wachezaji wenye viwango vya juu kutoka barani Afrika.

"Chama ni kiungo bora ambaye amewahi kuichezea ligi yetu hapa nchini, tunatamani siku moja atue Yanga, ni suala la muda, hakuna kisichowezekana," alisema Said.

Hata hivyo Yanga imeendelea kuwapandisha 'presha' mashabiki wa Simba baada ya Ofisa Habari wake, Haji Manara, kuonekana akiwa nchini Morocco, mahali ambapo Chama yuko akiichezea klabu ya RS Berkane.

Kwa sasa ligi imesimama kupisha kalenda ya kimataifa na itakaporejea, Simba itawafuata Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza mechi ikichezwa Novemba 19, mwaka huu wakati Yanga yenyewe itakwenda ugenini Lindi kuvaana na wenyeji Namungo FC.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >